JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A (GATCE) 2023

## UALIMU

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A (GATCE) 2023

# 610 UALIMU

*Kimechapishwa na:*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2023**

Haki zote zimehifadhiwa.

**YALIYOMO**

DIBAJI ... iv
1.0 UTANGULIZI ... 1
2.0 TATHMINI YA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA SWALI ... 2
2.1 SEHEMU A: Maswali ya Majibu Mafupi ... 2
2.1.1 Swali la 1: Ushauri na Unasihi ... 2
2.1.2 Swali la 2: Ushauri na Unasihi ... 4
2.1.3 Swali la 3: Upimaji katika Elimu ... 7
2.1.4 Swali la 4: Upimaji katika Elimu ... 10
2.1.5 Swali la 5: Ufundishaji ... 12
2.1.6 Swali la 6: Elimu ya Watu Wazima ... 15
2.1.7 Swali la 7: Nadharia za Kujifunza ... 18
2.1.8 Swali la 8: Upimaji katika Elimu ... 20
2.1.9 Swali la 9: Mtaala ... 23
2.1.10 Swali la 10: Uongozi wa Elimu Tanzania ... 26
2.2 SEHEMU B: Maswali ya Insha ... 28
2.2.1 Swali la 11: Makuzi na Ukuaji wa Mtoto ... 28
2.2.2 Swali la 12: Mtaala ... 32
2.2.3 Swali la 13: Upimaji katika Elimu ... 39
2.2.4 Swali la 14: Taaluma ya Ualimu ... 44
3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA MADA ... 48
4.0 HITIMISHO ... 48
5.0 MAPENDEKEZO ... 49
Kiambatisho cha pekee ... 50

## DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limetayarisha taarifa hii ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika mtihani wa Cheti Daraja la A katika somo la Ualimu mwaka 2023. Lengo la taarifa hii ni kutoa mrejesho wa ufaulu wa watahiniwa kwa walimu tarajali, wakufunzi, watunga sera, wakuza mitaala, na wadau wengine wa elimu kuhusu namna watahiniwa walivyojibu maswali mbalimbali.

Uchambuzi uliowasilishwa katika taarifa hii una lengo la kutoa uelewa zaidi juu ya sababu za watahiniwa kufanya vizuri, wastani, au vibaya katika mtihani huu. Kwa ujumla, ufaulu katika somo la Ualimu ulikuwa wa kiwango kizuri kwani watahiniwa wengi walitambua mahitaji ya swali kwa kuwa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada husika. Hawa walielewa vizuri dhana mbalimbali zilizotahiniwa, walikuwa na uwezo wa kujibu maswali kulingana na nyanja husika. Aidha, watahiniwa walikuwa na ujuzi wa kutosha katika uandishi wa insha. Vilevile, katika maswali yaliyokuwa na ufaulu wa wastani, watahiniwa walitoa hoja chache kuliko matakwa ya swali husika huku wengine wakichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi. Aidha, wengine walirudia hoja moja kwa namna tofauti.

Isitoshe, katika maswali yaliyokuwa na ufaulu hafifu, watahiniwa hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada zilizotahiniwa, dhana mbalimbali zinazohusiana na somo la Ualimu na matakwa ya swali. Aidha, watahiniwa hao walikosa umahiri wa kujieleza katika mtiririko unaoleta mantiki na kushindwa kuandika sehemu za utangulizi na hitimisho hususan katika maswali ya insha. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika maswali waliyojibu unatoa picha halisi ya mafanikio na changamoto zinazojitokeza katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Ualimu katika vyuo vya Ualimu Tanzania.

Ni matumaini ya Baraza la Mitihani la Tanzania kuwa mrejesho huu utawawezesha viongozi wa elimu, wakuu wa vyuo, wakufunzi na wanachuo kutumia mbinu muafaka ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Maboresho hayo yatasaidia kuinua kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika mitihani ijayo inayoandaliwa na Baraza la Mitihani la Tanzania.

Mwisho, Baraza la Mitihani la Tanzania linapenda kuwashukuru wadau wote waliohusika katika uchambuzi wa takwimu na kuandaa taarifa hii.

Dkt. Said A. Mohamed
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Mtihani wa somo la Ualimu kwa watahiniwa wa ngazi ya Astashahada uliofanyika mwezi Mei, 2023, uliandaliwa kwa kuzingatia Muhtasari wa somo la Ualimu wa mwaka 2009 ngazi ya Cheti Elimu ya Msingi. Mtihani huo ulikuwa na maswali 14, ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote katika sehemu A na B. Sehemu A ilikuwa na maswali 10 ya majibu mafupi, na kila swali lilikuwa na alama nne (04). Sehemu B ilikuwa na maswali manne (04) ya insha ambapo kila swali lilikuwa na alama 15.

Kwa ujumla, kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika somo la Ualimu kwa mwaka 2023 kilikuwa kizuri kwani watahiniwa 4,300 (99.86%) walikuwa na ufaulu wa wastani hadi mzuri. Kiwango hiki cha ufaulu kimepanda ikilinganishwa na mwaka 2022 kama inavyoonekana katika jedwali la pekee.

**Jedwali la Pekee: Ufaulu wa Watahiniwa kwa kila Daraja**

| Mwaka | Watahiniwa Waliofanya | Asilimia ya Watahiniwa Waliofaulu (%) | Madaraja | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | A | B | C | D | F |
| 2022 | 3,272 | 99.85 | 22 | 804 | 2,272 | 146 | 5 |
| 2023 | 4,354 | 99.86 | 17 | 603 | 3,128 | 552 | 6 |

Jedwali la pekee linaonesha kuwa asilimia 99.86 ya watahiniwa walifaulu kwa mwaka 2023. Jedwali linaonesha kuwa ufaulu uliongezeka kwa asilimia 0.01 ikilinganishwa na mwaka 2022.

Ufaulu wa watahiniwa umegawanywa katika viwango vitatu ambavyo ni ufaulu mzuri, wastani, na hafifu. Ufaulu mzuri unaanzia alama 70 hadi 100, wastani alama 40 hadi 69 na hafifu alama 0 hadi 39. Aidha, kiwango cha ufaulu kwa kila swali katika sehemu A ni *kizuri* ikiwa watahiniwa watapata alama 3 hadi 4, kiwango cha *wastani* alama 2 na 2.5, na kiwango *hafifu* alama 0 hadi 1.5. Kwa maswali ya sehemu B, kiwango cha ufaulu katika kila swali ni *kizuri* ikiwa watahiniwa watapata 10.5 hadi 15, kiwango cha *wastani* alama 6 hadi 10, na kiwango *hafifu* alama 0 hadi 5.5.

Katika kufanya uchambuzi na kufasiri ufaulu wa watahiniwa, chati na rangi zimetumika ili kufafanua ufaulu husika. Rangi ya kijani inawakilisha ufaulu mzuri, njano ufaulu wa wastani, na nyekundu ufaulu hafifu. Uchambuzi huu unalenga kuonesha jinsi watahiniwa walivyojibu maswali katika mtihani wa somo la Ualimu. Sampuli za majibu ya watahiniwa zimeambatishwa ili kuonesha majibu waliyofanya vibaya na waliyofanya vizuri. Aidha, taarifa inaonesha sababu zilizowafanya baadhi ya watahiniwa kupata au kutopata alama za juu katika majibu ya maswali kwa mada zilizotahiniwa. Hivyo, uchambuzi huu utasaidia kuimarisha

ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Ualimu kwa mada hizo ili kuongeza ufaulu wa watahiniwa katika mitihani yao.


## 2.0 TATHMINI YA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA SWALI

### 2.1 SEHEMU A: Maswali ya Majibu Mafupi

Maswali katika sehemu A yalitoka katika mada saba (7) ambazo ni *Ushauri na Unasihi, Upimaji katika Elimu, Ufundishaji, Elimu ya Watu Wazima, Nadharia za Kujifunza, Mtaala* na *Uongozi wa Elimu Tanzania*. Kila swali lilikuwa na alama nne (4) hivyo, kufanya jumla ya alama 40.

#### 2.1.1 Swali la 1: Ushauri na Unasihi

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubainisha mambo manne ya kuzingatia inapotumika mbinu ya mshauri kuwa kiini cha ushauri wakati wa unasihi. Watahiniwa 4,354 (100%) walijibu swali hili. Takwimu za ufaulu wa watahiniwa katika swali hili zinaonesha kuwa watahiniwa 441 (10.1%) walipata alama 0 hadi 1.5, watahiniwa 2,419 (55.6%) walipata alama 2 hadi 2.5, na watahiniwa 1,494 (34.3%) walipata alama 3 hadi 4. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 1.





**Chati Na. 1:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 1*

Chati Na. 1 inaonesha kuwa asilimia 10.1 ya watahiniwa walipata alama 0 hadi 1.5, asilimia 55.6 walipata alama 2 hadi 2.5, na asilimia 34.3 walipata alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa asilimia 89.9% ya watahiniwa walipata alama 2 hadi 4.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 2,419 (55.6%) waliopata alama 2 hadi 2.5 walikuwa na dosari mbalimbali katika hoja zao. Hivyo, walishindwa kupata alama zote nne. Wengi wao katika kundi hili walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi; huku wengine wakitoa hoja pungufu hivyo, walishindwa kupata alama za juu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika hoja sahihi lakini pungufu kama vile *kuzingatia mahali au sehemu ya kufanyia ushauri na unasihi,* na *kuzingatia muda wa kufanya ushauri na unasihi.* Mtahiniwa mwingine aliandika hoja kama vile *kuwa mkweli na muwazi, kutunza siri, kuwa mpole, kuwa mdadisi wa kuibua maswali,* na *kuheshimu mawazo ya mteja*. Hoja za mtahiniwa huyo zilikuwa dhaifu hasa hoja ya kwanza na ya tatu jambo linaloashiria ukosefu wa maarifa ya kutosha juu ya mada husika. Majibu hayo yanaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha.


Vilevile, takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 1,494 (34.3%) waliopata alama 3 hadi 4 walielewa matakwa ya swali na walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya *Ushauri na Unasihi,* hususan kipengele cha *mambo ya kuzingatia inapotumika mbinu ya mshauri kama kiini cha ushauri wakati wa unasihi*. Watahiniwa 1,245 (28.6%) walikuwa na maarifa ya kutosha na walielewa vema matakwa ya swali, hivyo, walitoa hoja sahihi kama vile *kuwa mwaminifu na kutunza siri kwa wale unao wapatia ushauri, kumhakikishia anayepewa ushauri usalama kwa kutotoa siri zake, kutoa ushauri kulingana na tatizo,* na *kuwa na ubunifu wa kutatua changamoto za walengwa*. Kielelezo Na. 1.1 ni sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali la 1.


1 i) kumwezesha mteja kubaini kuwa ana tatizo.
ii) Kulichukua tatizo la mteja kama la kwake
iii) Kufanya uchunguzi ili kuweza kubaini chanzo cha tatizo.
iv) kupendekeza mbinu/njia ambazo mteja atatumia kutatua tatizo hilo.

**Kielelezo Na. 1.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 1.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 441 (10.1%) waliokuwa na alama 0 hadi 1.5 hawakuelewa matakwa ya swali. Hivyo, walitoa hoja zisizo sahihi. Kati yao, watahiniwa 35 (0.8%) walipata alama sifuri kwani badala ya kubainisha mambo manne ya kuzingatia inapotumika mbinu ya mshauri kuwa kiini cha ushauri wakati wa unasihi, walibainisha sifa anazopaswa kuwa nazo mnasihi. Wengine walitoa hoja zinazohusiana na matayarisho kabla ya

unasihi kama vile *kuwasili kwa mteja, kufahamiana,* na *kikao cha unasihi mwisho wa kikao kilichopita.* Mtahiniwa mwingine alitoa hoja zinazohusu mbinu atumiazo mnasihi kama vile *kubaini tatizo, kujua chanzo cha tatizo, njia za kuzuia tatizo,* na *namna ya kuzuia tatizo lisitokee tena.* Mtahiniwa mwingine alitoa hoja dhaifu kama vile *umri wa walengwa, maswali na majibu, jua chanzo cha tatizo,* na *epuka maswali ya kuudhi.* Majibu hayo ya watahiniwa yanaonesha kuwa hawakuwa na uelewa kabisa kuhusu mambo ya kuzingatia inapotumika mbinu ya mshauri kuwa kiini cha ushauri wakati wa unasihi. Kielelezo Na. 1.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutoa majibu sahihi katika swali hili.



1
(i). Utangulizi.
(ii). Dhumuni.
(iii) kutafuta suluhisho.
(iv). Hitimisho.

**Kielelezo Na. 1.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 1.

Katika Kielelezo Na. 1.2, mtahiniwa aliandika mambo yanayohusu mpangilio wa uandishi katika kikao cha unasihi badala ya mambo ya kuzingatia inapotumika mbinu ya mshauri kama kiini cha ushauri wakati wa unasihi.

### 2.1.2 Swali la 2: Ushauri na Unasihi


Swali hili lilimtaka mtahiniwa kueleza kwa ufupi hoja nne zinazoonesha ufanano kati ya ushauri nasaha wa jadi na ushauri nasaha wa kisasa. Jumla ya watahiniwa 4,354 (100%) walijibu swali hili. Takwimu za ufaulu wa watahiniwa katika swali hili zinaonesha kuwa watahiniwa 2,196 (50.4%) walipata alama 3 hadi 4, watahiniwa 931 (21.4%) walipata alama 2 hadi 2.5, na watahiniwa 1,227 (28.2%) walipata alama 0 hadi 1.5. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 2.




**Chati Na. 2:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 2*


Chati Na. 2 inaonesha kuwa asilimia 50.4 ya watahiniwa walipata alama 3 hadi 4, asilimia 21.4 walipata alama 2 hadi 2.5, na asilimia 28.2 walipata alama 0 hadi 1.5. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa asilimia 71.8 ya watahiniwa walipata alama 2 hadi 4.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa kati ya watahiniwa 2,196 (50.4%) waliopata alama 3 hadi 4, watahiniwa 1,065 (24.5%) walipata alama zote nne kwa kuwa waliweza kueleza vizuri ufanano kati ya ushauri nasaha wa jadi na ushauri nasaha wa kisasa. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana nzima ya *ushauri na unasihi.* Hivyo, walitoa hoja sahihi na kukidhi matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja sahihi kama vile *zote hulenga kutatua tatizo fulani, kwa zote mbili mteja ndio anafanya maamuzi, kwa zote mbili hutolewa sehemu maalum,* na *zote mbili hufanywa na watu maalumu.* Pia, mtahiniwa mwingine alitoa hoja sahihi kama vile *aina zote za ushauri nasaha hulenga kutatua tatizo au changamoto aliyonayo mteja, aina zote za ushauri nasaha huzingatia kanuni na taratibu za kumshauri mteja, aina zote za ushauri nasaha zinalenga kuzuia athari hasi,* na *aina zote za ushauri nasaha hufanyika sehemu maalum au faragha.* Kielelezo Na. 2.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.


i) Ushauri nasaha wa jadi na wakisasa wote-unahimiza misingi ya maadili.
ii) Ushauri nasaha wa jadi na wakisasa wote-mnasihi lazima awe na siri za mambo yote-aliyoyafanyia unasihi.
iii) Ushauri nasaha wa jadi na wa kisasa wote unafanyika sehemu ya faragha.
iv) Ushauri nasaha wa jadi na wa kisasa wote unahitaji matayarisho kabla ya kuanza unasihi.

**Kielelezo Na. 2.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 2.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 1,227 (28.2%) waliopata alama 0 hadi 1.5 kati yao, watahiniwa 644 (14.8%) walipata alama sifuri. Baadhi ya waliopata alama sifuri waliandika tofauti kati ya ushauri nasaha wa jadi na wa kisasa badala ya ufanano wa ushauri nasaha wa jadi na wa kisasa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika kuwa *ushauri nasaha wa jadi hutolewa na viongozi wa jamii fulani na ushauri nasaha wa kisasa hutolewa na mtaalaumu wa unasihi, ushauri nasaha wa jadi haina muda maalumu na ushauri nasaha wa kisasa hutolewa kwa kuzingatia muda, ushauri nasaha wa jadi hutolewa sehemu yoyote mfano nyumbani na ushauri nasaha wa kisasa hutolewa katika vituo maalum,* na *ushauri nasaha wa jadi hutolewa bila utaratibu wowote na ushauri nasaha wa kisasa hutolewa na mnasihi ambaye huwa chanzo cha unasihi*. Mtahiniwa mwingine aliandika *ushauri nasaha wa jadi ulikuwa unatumiwa zamani wakati ushauri nasaha wa kisasa huu hutumiwa sasa na napendwa na wengi, ushauri nasaha wa jadi hutumia mbinu za zamani tu na wa kisasa hutumia mbinu za kisasa tu, ushauri nasaha wa jadi hutolewa eneo lolote wakati ushauri nasaha wa kisasa hutolewa sehemu maalumu na muda maalumu,* na *ushauri nasaha wa jadi hutolewa na mtu yeyote wakati ushauri nasaha wa kisasa hutolewa na mtaalamu.* Majibu ya watahiniwa katika kundi hili yanaonesha kuwa walikuwa na uelewa wa dhana hizo isipokuwa hawakuelewa matakwa ya swali. Kielelezo Na. 2.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutoa majibu sahihi katika swali la 2.



| 2 | i/ Ushauri nasaha jadi ni kupewa ushauri wa dak |
|---|---|
| | tari kwa kuumwa mgonjwa aliyekata tamaa. Ush |
| | auri nasaha wakisasa, kupewa ushauri wa mtu |
| | yeyote yule anayemzunguka katika famii. |
| | |
| | ii/ Ushauri nasaha jadi kupewa ushauri kwa mgon |
| | jwa wa ukimwi wa mda mrefu. lakini ushauri nasaha |
| | kisasa upewa ushauri kwa yule anayeishi nae hata |
| | majumbani. |
| | |
| | iii/ Ushauri nasahajadi; kupewa ushauri kuzingatia |
| | daktari. lakini ushauri nasaha kisasa kupewa ushau |
| | ri kwa kuzingatia mtu mwenye uelewa na kuji |
| | heshimu. |


**Kielelezo Na. 2.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 2.

Katika Kielelezo Na. 2.2, mtahiniwa alieleza tofauti ya ushauri nasaha wa jadi na ushauri nasaha wa kisasa badala ya kueleza ufanano wa ushauri nasaha wa jadi na ule wa kisasa.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 931 (21.4%) waliopata alama 2 hadi 2.5 walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi. Wengine walifafanua sababu pungufu au zisizojitosheleza, hivyo, kupata alama za wastani. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza hoja mbili badala ya nne ambazo ni *hutolewa katika muda maalum* na *hutolewa katika mazingira tulivu*. Pia, alitoa hoja moja ambayo siyo sahihi kuwa *ushauri nasaha wa jadi hutolewa sehemu ya wazi wakati ushauri nasaha wa kisasa hutolewa kwenye chumba kilicho wazi au sehemu ya wazi.* Mtahiniwa mwingine, alieleza kuwa *vyote vinatoa huduma ya unasihi, vyote vinatoa mafunzo kwa wahitaji, vyote vinatatua changamoto mbalimbali* na *vyote vinarekebisha tabia na mwenendo mbaya wa binadamu*. Katika hoja alizotoa mtahiniwa, hoja ya kwanza ilikuwa sahihi na hoja zingine zilikuwa na madhaifu. Hivyo, alipata alama kama ilivyostahili. Majibu hayo yanaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu ufanano kati ya ushauri nasaha wa kisasa na wa jadi.

### 2.1.3 Swali la 3: Upimaji katika Elimu


Swali hili lilimtaka mtahiniwa kufafanua ngazi nne za Nyanja ya Stadi kwa kufuata mtiririko kutoka ngazi ya chini hadi ngazi ya juu. Jumla ya watahiniwa 4,354 (100%) walijibu swali hili. Takwimu za ufaulu wa watahiniwa katika swali hili zinaonesha kuwa watahiniwa 3,761 (86.4%) walipata alama 0 hadi 1.5, watahiniwa 240 (5.5%) walipata alama 2 hadi 2.5, na watahiniwa 353 (8.1%) walipata alama 3 hadi 4. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 3.




**Chati Na. 3:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 3*

Chati Na. 3 inaonesha kuwa asilimia 86.4 ya watahiniwa walipata alama 0 hadi 1.5, asilimia 5.5 walipata alama 2 hadi 2.5, na asilimia 8.1 walipata alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa hafifu kwa kuwa asilimia 13.6 ya watahiniwa ndiyo waliopata alama 2 hadi 4.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa kati ya watahiniwa 3,761 (86.4%) waliopata alama 0 hadi 1.5, watahiniwa 3,186 (73.2%) walipata alama sifuri kutokana na kuandika hoja zisizo sahihi jambo linaloashiria ukosefu wa maarifa juu ya ngazi za nyanja ya stadi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa ngazi zisizo sahihi kama vile *upokeaji; katika ngazi hii mwanafunzi hutakiwa kuwa na uwezo wa kupokea mambo anayokuwa akifundishwa, ngazi ya kuthubutu; hupelekea mwanafunzi kujifunza, ngazi ya matumizi; hii huonekana pale ambapo mwalimu ameshafundisha,* na *ngazi ya tathmini hapa humtaka mwanafunzi kuweza kujua hali halisi ya jambo.* Mtahiniwa mwingine alitoa hoja kama vile *mwitikio, utayari, kuthubutu,* na *uzoeshi au uwezo wa kufikiri*. Mtahiniwa mwingine alifafanua stadi za mawasiliano kama vile *kusikiliza, kuzungumza, kusoma,* na *kuandika* badala ya kufafanua ngazi za nyanja ya stadi kwa kufuata mtiririko kutoka ngazi ya chini hadi ngazi ya juu. Kielelezo Na. 3.1 ni sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali hili.




| | |
|---|---|
| 3 | (i) Ujuzi |
| | (ii) Maarifa |
| | (iii) Mielekeo |
| | (iv) Stadi |

**Kielelezo Na. 3.1:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 3.

Katika Kielelezo Na. 3.1, mtahiniwa alifafanua kwa kuchanganya nyanja na ngazi za upimaji katika elimu badala ya kufafanua ngazi za nyanja ya stadi ambazo ni ngazi ya uchunguzi, kuiga, mazoezi na kuthaminisha.

Vilevile, uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa kati ya watahiniwa 353 (8.1%) waliopata alama 3 hadi 4, watahiniwa 26 (0.6%) walipata alama zote nne kwa sababu walikua na maarifa ya kutosha katika mada ya *Upimaji katika Elimu*. Watahiniwa hao walifafanua ngazi nne za nyanja ya stadi kwa kufuata mtiririko sahihi kutoka ngazi ya chini hadi ngazi ya juu. Walifafanua ngazi husika kwa kufuata mtiriko sahihi kama vile *uchunguzi; ambapo mtoto huanza kuchunguza vitu mbalimbali katika ujifunzaji wake ili aelewe zaidi, kuiga; ambapo mtoto hutaka kuiga namna alivyoona mambo yanavyofanyika,* na *ngazi ya mazoezi ambayo huanza kufanya mazoezi ili aweze kuyamudu mambo hayo na kuwa mahiri katika kuyatenda.* Kielelezo Na. 3.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.


3

Ngazi za Nyanja ya Stadi au Vitendo

i) Uchunguzi

Mtu katika ngazi hii anachunguza jambo kwa umakini kama lina faida au hasara kwake.

ii) Kuiga

Katika ngazi hii mtu huanza kuiga mambo au vitu mbalimbali baada ya kufanya uchunguzi

iii) Mazoezi

Baada ya kufanya uchunguzi wa jambo na kuiga mtu anafanya mazoezi ya Mambo au vitu aliyoyaiga.

iv) Uthamini

Baada ya kuiga na kufanya mazoezi ya jambo mtu anathamini kile alichokifanyia mazoezi


**Kielelezo Na. 3.2:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 3.

Aidha, watahiniwa 240 (5.5%) waliopata alama 2 hadi 2.5 walikuwa na mapungufu mbalimbali katika hoja zao. Kwa mfano, kuchanganya hoja sahihi na zisizo sahihi, kutoa hoja pungufu ya zilizohitajika na kutoa hoja zenye usahihi kidogo. Hivyo, walipata alama za wastani. Kwa mfano, mtahiniwa mmojawapo aliweza kufafanua ngazi mbili za nyanja ya vitendo kwa usahihi kama ifuatavyo: *Ngazi ya kuiga ambayo ni ngazi ya pili katika nyanja ya stadi ambapo mwanafunzi hufanya kwa kuiga yale aliyojifunza kwa mwalimu* na *ngazi ya mazoezi ambayo ni ngazi ya tatu katika nyanja ya stadi ambapo mwanafunzi hufanya yale aliyoyaiga kwa kufanya mazoezi kuhusianisha na alichokifanya mwalimu*. Aidha, katika ngazi ya uchunguzi mtahiniwa huyo alishindwa kutoa maelezo sahihi kwa kuandika

kuwa *uchunguzi unahusisha mwanafunzi kupimwa kama ana stadi ya kuchunguza yale aliyojifunza.* Pia, alishindwa kutaja ngazi ya juu ya nyanja ya stadi ambayo ni *kuthaminisha* na badala yake aliandika kuwa *tathmini ni ngazi ya mwisho au ya juu ambapo mwalimu hufanya tathmini*. Mtahiniwa mwingine alichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi kama vile *ngazi ya uchunguzi, ngazi ya kuiga, ngazi ya matumizi,* na *ngazi ya tathmini.* Mtahiniwa huyu katika hoja ya tatu na ya nne aliandika *ngazi ya matumizi* na *ngazi ya tathmini* ambazo siyo sahihi. Majibu hayo yanaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu nyanja ya stadi au ujuzi.

### 2.1.4 Swali la 4: Upimaji katika Elimu

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubainisha mambo manne muhimu katika kipengele cha taaluma ambayo yanatakiwa kuingizwa kwenye kumbukumbu za maendeleo ya wanafunzi. Jumla ya watahiniwa 4,354 (100%) walijibu swali hili. Takwimu za ufaulu wa watahiniwa katika swali hili zinaonesha kuwa watahiniwa 3,446 (79.1%) walipata alama 0 hadi 1.5, watahiniwa 586 (13.5%) walipata alama 2 hadi 2.5, na watahiniwa 322 (7.4%) walipata alama 3 hadi 4. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 4.




**Chati Na. 4:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 4*

Chati Na. 4 inaonesha kuwa asilimia 79.1 ya watahiniwa walipata alama 0 hadi 1.5, asilimia 13.5 walipata alama 2 hadi 2.5, na asilimia 7.4 walipata alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa hafifu kwa kuwa asilimia 20.9 ya watahiniwa ndio waliopata alama 2 hadi 4.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa kati ya watahiniwa 3,446 (79.1%) waliopata alama 0 hadi 1.5, watahiniwa 707 (16.2%) walipata alama sifuri kwa vile hawakuwa na maarifa kuhusu dhana ya uwekaji kumbukumbu za maendeleo ya wanafunzi. Hivyo, walitoa hoja zisizoendana na swali kama vile *kuwepo kwa ufaulu mzuri wa mitihani, kuwepo kwa kushika nafasi nzuri kitaifa, kuwepo kwa wanafunzi wanaoendelea na ngazi za juu,* na *kuwepo kwa ufaulu mzuri wa wanafunzi.* Pia, mtahiniwa mwingine alibainisha mambo muhimu ya kuingizwa kwenye kumbukumbu za maendeleo ya mwanafunzi kuwa ni *maarifa, ujuzi, stadi,* na *tathmini.* Mtahiniwa mwingine alibainisha taarifa binafsi za mwanafunzi kama vile *jina la shule husika, jina la mwanafunzi, darasa husika la mwanafunzi,* na *umri wa mwanafunzi* badala ya kumbukumbu za maendeleo ya wanafunzi. Kielelezo Na. 4.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.

**4** Mambo ambayo yanatakiwa kuingizwa kwenye kumbukumbu ya maendeleo ya Mwanafunzi ~~At~~ kitaaluma ni
Kumbukumbu, ili kujua kama Mwanafunzi anauwezo wa kukumbuka yale aliyofundishwa.
Vitendo, ili kujua kama Mwanafunzi anauwezo wa kutenda kutokana na aliyofundisha.
Utambuzi ili kujua kama Mwanafunzi anaweza kutambua vitu tofauti kulingana na aliyofundishwa,
Uelekeo, ili kujua kama mwanafunzi anaelekea toka alipoanza kujifunza mpaka alipofikia,


**Kielelezo Na. 4.1:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 4.

Katika Kielelezo Na. 4.1, mtahiniwa alibainisha Nyanja za Upimaji badala ya mambo muhimu ya kuingizwa kwenye kumbukumbu za maendeleo ya wanafunzi.

Aidha, watahiniwa 586 (13.5%) waliopata alama 2 hadi 2.5 walishindwa kutoa hoja zote kwa usahihi na baadhi yao walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmojawapo aliandika hoja sahihi kama vile *alama za*

*mitihani yake* na *maoni ya mwalimu juu ya ufaulu wake kama kajitahidi ama aongeze bidii*. Hoja zisizo sahihi zilizotolewa na mtahiniwa huyo ni *tabia ya mwanafunzi kama ni nzuri, mbaya au ya kuridhisha,* na *mwonekano wake kama ni msafi au nadhifu na kama ni mchafu*. Mtahiniwa mwingine alitoa hoja mbili sahihi ambazo ni *matokeo ya majaribio ya masomo mbalimbali* na *nafasi anayoipata mwanafunzi katika kila mtihani wanaofanya shuleni au kikata*. Pia, alitoa hoja mbili zisizo sahihi ambazo ni *kadi ya maeneleo ya mwanafunzi* na *nidhamu na mwenendo.* Hivyo, alipata alama za wastani. Majibu haya yanaonesha kuwa watahiniwa katika kundi hili hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mambo ya kitaaluma yanayotakiwa kuwekwa kwenye kumbukumbu za maendeleo ya mwanafunzi.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 322 (7.4%) waliopata alama 3 hadi 4 walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu uwekaji wa kumbukumbu za maendeleo ya wanafunzi, hivyo, walieleza kwa usahihi mambo muhimu ya kuzingatia katika uwekaji wa kumbukumbu za maendeleo ya mwanafunzi kitaaluma. Watahiniwa 86 (2%) waliopata alama zote nne walitoa hoja sahihi. Majibu ya watahiniwa hao yalidhihirisha kuwa walielewa matakwa ya swali na walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu uwekaji wa kumbukumbu za maendeleo ya wanafunzi. Mtahiniwa mmoja alitoa hoja kama vile *ufaulu wa masomo, matumizi ya lugha, mwandiko,* na *maoni ya mzazi*. Mtahiniwa mwingine alitoa hoja kama vile *matokeo ya mitihani, kazi za vikundi, kazi mradi,* na *mazoezi mbalimbali ya darasani*. Kielelezo Na. 4.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.



4
i) Matokeo ya mitihani
ii) Matokeo ya majaribio
iii) Maoni ya mwalimu
iv) Maoni ya Mzazi /mlezi

**Kielelezo Na. 4.2:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 4.

### 2.1.5 Swali la 5: Ufundishaji

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kueleza kwa ufupi faida mbili na hasara mbili za kutumia mbinu ya kusoma kwa sauti katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Jumla ya watahiniwa 4,354 (100%) walijibu swali hili. Takwimu za ufaulu wa watahiniwa katika swali hili zinaonesha kuwa watahiniwa 71 (1.6%) walipata alama 0 hadi 1.5, watahiniwa 2,896 (66.5%) walipata alama 2 hadi 2.5, na

watahiniwa 1,387 (31.9%) walipata alama 3 hadi 4. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 5.





**Chati Na. 5:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 5*

Chati Na. 5 inaonesha kuwa asilimia 1.6 ya watahiniwa walipata alama 0 hadi 1.5, asilimia 66.5 walipata alama 2 hadi 2.5, na asilimia 31.9 walipata alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa asilimia 98.4 ya watahiniwa walipata alama 2 hadi 4.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 2,896 (66.5%) waliopata alama 2 hadi 2.5 walikuwa na mapungufu mbalimbali katika majibu yao kama vile kuchanganya hoja sahihi na zisizo sahihi, kutoa hoja dhaifu na wengine kushindwa kuelezea faida mbili na hasara mbili za kutumia mbinu ya kusoma kwa sauti katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji na hivyo, kupata alama za wastani. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja sahihi kwa upande wa faida kuwa ni *kukuza stadi ya kusoma na kuelewa zaidi* na *kubaini matatizo waliyonayo wanafunzi katika utamkaji wa maneno mfano lala atatamka rara*. Hata hivyo, kwa upande wa hasara ya kutumia mbinu ya kusoma kwa sauti alitoa hoja dhaifu kama vile *huwachosha wanafunzi* na *ni usumbufu kwa wengine kutokana na sauti inayosikika*. Mtahiniwa mwingine alieleza kwa usahihi faida kuwa ni *humjengea mwanafunzi uwezo wa kufuata kanuni za uandishi* na *humjengea mwanafunzi hali ya kujiamini*. Aidha, alieleza hasara zisizo sahihi kama vile *kuwasumbua wengine* na *haitunzi kumbukumbu*. Majibu hayo yanaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mbinu ya kusoma kwa sauti.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 1,387 (31.9%) waliopata alama 3 hadi 4 waliweza kueleza kwa ufupi faida mbili na hasara mbili za kutumia mbinu ya kusoma kwa sauti katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Watahiniwa 1,167 (26.8%) waliopata alama zote nne walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mbinu ya kusoma kwa sauti. Mtahiniwa mmojawapo alieleza kwa usahihi faida kuwa ni *huimarisha stadi ya kuzungumza kwa kuwa wanafunzi hujifunza namna ya kutamka maneno kwa usahihi* na *husaidia kugundua baadhi ya wanafunzi wenye matatizo katika usomaji wa maneno mbalimbali*. Pia, alieleza hasara za mbinu hiyo kuwa ni *sio wanafunzi wote wanaosoma, baadhi ya wanafunzi huwa ni wategaji wakati wenzao wanasoma na dhana inaweza isieleweke kwa wanafunzi,* na *wanafunzi wanaweza wasielewe kile kinachosomwa au wanachokisoma*. Kielelezo Na. 5.1 ni sampuli ya majibu sahihi katika swali hili.


5

Kusoma kwa sauti ni mbinu anayoweza kuitumia mwalimu kwa kumwambia mwanafunzi asome na wengine kusikiliza kinachosomwa.

Faida za kusoma kwa sauti

i) Humfanya mwanafunzi kuongeza umakini katika kusikiliza kinachosomwa.

ii) Huokoa muda kutokana na wanafunzi kusikiliza wote kwa pamoja.

Hasara za kusoma kwa sauti


i) Wanafunzi kushindwa kuuliza maswali kama kuna sehemu hajaelewa.

ii) Baadhi ya wanafunzi wenye matatizo ya milango ya fahamu huumia kutokana na sauti ile kuwa yajuu sana.

**Kielelezo Na. 5.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 5.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 71 (1.6%) waliopata alama 0 hadi 1.5 walikuwa na udhaifu katika kuelewa matakwa ya swali, kuandika hoja pungufu hasa zinazohusu faida za mbinu ya kusoma kwa sauti na kushindwa kuandika hasara za mbinu hiyo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja zisizo sahihi upande wa faida ambazo ni *inarahisisha mchakato wa*

*ufundishaji na ujifunzaji* na *inamsaidia mwalimu kufikia lengo au shughuli mahususi*. Pia, alieleza hasara zisizo sahihi kuwa ni *hupoteza usikivu kwa wanafunzi wengine* na *wanafunzi kukosa umakini*. Mtahiniwa mwingine alitoa maelezo kama vile *kutambulika kwa jambo husika linalosomwa* na *kusikia vizuri kwa jambo*. Aidha, alitoa kasoro zisizo sahihi kama vile *kutohifadhi kumbukumbu ya jambo husika kwa haraka* na *husababisha usumbufu kwa wengine*. Kielelezo Na. 5.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.



5 Faida za Kusoma Kwa sauti
i. Husaidia Mwanafunzi Mwenye Mahitaji Maalumu Kuweza Kujifunza Kwa Ufasaha Mfano Mawanafunzi hasiye sikia vizuri (Kiziwi)
ii Husaidia Mwanafunzi Kuwa Mdadisi.
Hasara zake ni:
i Huwa ni Kelele Kwa baadhi ya Wanafunzi
ii Chanzo Cha Migogoro Mwengeni Mwa Wanafunzi na Walimu

**Kielelezo Na. 5.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 5.

Katika Kielelezo Na. 5.2, mtahiniwa aliandika hoja zisizo sahihi kuhusu faida na hasara za kutumia mbinu ya kusoma kwa sauti katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

### 2.1.6 Swali la 6: Elimu ya Watu Wazima


Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kutoa matukio manne yaliyofanyika kama sehemu ya kuimarisha elimu ya watu wazima nchini Tanzania. Jumla ya watahiniwa 4,354 (100%) walijibu swali hili. Takwimu za ufaulu wa watahiniwa katika swali hili zinaonesha kuwa watahiniwa 2,559 (58.8%) walipata alama 0 hadi 1.5, watahiniwa 771 (17.7%) walipata alama 2 hadi 2.5, na watahiniwa 1,024 (23.5%) walipata alama 3 hadi 4. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 6.




**Chati Na. 6:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 6*

Chati Na. 6 inaonesha kuwa asilimia 58.8 ya watahiniwa walipata alama 0 hadi 1.5, asilimia 17.7 walipata alama 2 hadi 2.5, na asilimia 23.5 walipata alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu wa wastani kwa kuwa asilimia 41.2 ya watahiniwa walipata alama 2 hadi 4.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa kati ya watahiniwa 2,559 (58.8%) waliopata alama 0 hadi 1.5, watahiniwa 652 (15%) walipata alama sifuri kwa vile hawakuwa na kumbukumbu yoyote kuhusu matukio yaliyofanyika nchini Tanzania kama sehemu ya kuimarisha elimu ya watu wazima. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja zisizo sahihi kama vile *kujikwamua katika hali duni ya maisha, kuwafundisha kutunza mazingira na elimu ya afya zetu, kuwafundisha kushiriki katika uongozi wa serikali,* na *walifundishwa uzalishaji mali*. Pia, mtahiniwa mwingine alitoa hoja zisizoendana na matakwa ya swali kama vile *uchaguzi wa masomo anayohitaji kuyasoma, kutokuwepo kwa uvaaji wa sare, kuwapatia nafasi ya kuheshimiwa,* na *kusikilizwa juu ya maoni yao.* Majibu hayo ya watahiniwa yanaonesha kuwa hawakuwa na maarifa kuhusu matukio yaliyofanyika kama sehemu ya kuimarisha elimu ya watu wazima nchini Tanzania. Kielelezo Na. 6.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.



6

(i) Katika kazi.
(ii) Katika Demokrasia.
(iii) Katika kuthaminiana na kujaliana yaani utu.
(iv) Katika Ujenzi wa Maendeleo ya famii

**Kielelezo Na. 6.1:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali 6.

Katika Kielelezo Na. 6.1, mtahiniwa alibainisha mambo ya kijamii ambayo mtu mzima anaweza akashiriki badala ya kubainisha matukio yaliyofanyika kama sehemu ya kuimarisha elimu ya watu wazima nchini Tanzania.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa kati ya watahiniwa 1,024 (23.5%) waliopata alama 3 hadi 4, watahiniwa 555 (12.7%) walipata alama zote nne. Watahiniwa hao waliweza kubainisha kwa usahihi matukio manne yaliyofanyika kama sehemu ya kuimarisha elimu ya watu wazima nchini Tanzania. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja sahihi kama vile *kuanzishwa kwa idara ya elimu ya watu wazima, kuanzishwa kwa kampeni mbalimbali mfano mtu ni afya, kuanzishwa kwa Chuo Kikuu Huria ili kuendeleza elimu ya watu wazima,* na *kuanzishwa kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ili kupokea watu wazima.* Aidha, mtahiniwa mwingine alitoa hoja sahihi kama vile *kuanzishwa kwa kampeni mbalimbali za kufuta ujinga kwa mfano misitu ni mali, kuanzishwa kwa mabaraza ya wafanyakazi, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kupokea wanafunzi watu wazima, kuanzishwa kwa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima,* na *kuanzishwa kwa vyuo vya maendeleo vya kati*. Majibu hayo ya watahiniwa yanaonesha kuwa walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu jitihada zilizofanyika kuimarisha elimu ya watu wazima nchini Tanzania. Kielelezo Na. 6.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.


6


(i) Chuo Kikuu cha Dares Salaam kuanzo kupokea wanafunzi wengi watu wazima
(ii) Kuanzishwa kwa chuo kikuu Huria
(iii) Kuanzishwa kwa mabaraza ya wafanyakazi
(iv) Kuanzishwa kwa sera mbalimbali za kufuta ujinga kama vile Jenga Afya, Misitu ni mali.

**Kielelezo Na. 6.2:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 6.

Aidha, watahiniwa 771 (17.7%) waliopata alama 2 hadi 2.5 waliandika hoja pungufu ya zilizohitajika kwenye swali na wengine walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika hoja sahihi ambazo ni *kuongezeka kwa maktaba za umma* na *kupanuliwa kwa shahada za vyuo*. Aidha, alitoa hoja zisizo sahihi kama vile *kutiliwa kwa mkazo masomo ya sayansi na kilimo katika shule za sekondari* na *elimu ya watu wazima kuwa kama sehemu ya kazi.* Vilevile, mtahiniwa mwingine aliandika hoja sahihi kama vile *kuanzishwa kwa taasisi ya utoaji wa elimu ya watu wazima* na *kuanzishwa vyuo vya maendeleo ya wananchi*. Kwa upande mwingine, mtahiniwa huyo alitoa hoja zisizo sahihi kama vile *kuanzishwa kwa sera ya nchi ya ujamaa na kujitegemea* na *kutolewa kwa mafunzo ya elimu ya kujitegemea*. Majibu hayo yanaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Elimu ya Watu Wazima nchini Tanzania.

### 2.1.7 Swali la 7: Nadharia za Kujifunza

Swali hili lilimtaka mtahiniwa atumie hoja nne kueleza kwa ufupi jinsi elimu inavyoweza kutumika kama chombo cha ukandamizaji kama ilivyoelezwa na Paulo Freire. Jumla ya watahiniwa 4,354 (100%) walijibu swali hili. Takwimu za ufaulu wa watahiniwa katika swali hili zinaonesha kuwa watahiniwa 4,338 (99.6%) walipata alama 0 hadi 1.5, watahiniwa 5 (0.1%) walipata alama 2 hadi 2.5, na watahiniwa 11 (0.3%) walipata alama 3 hadi 4. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na.7.





**Chati Na. 7:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 7*

Chati Na. 7 inaonesha kuwa asilimia 99.6 ya watahiniwa walipata alama 0 hadi 1.5, asilimia 0.1 walipata alama 2 hadi 2.5, na asilimia 0.3 walipata alama 3 hadi 4.

Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu hafifu kwani asilimia 0.4 ya watahiniwa ndiyo waliopata alama 2 hadi 4.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 4,338 (99.6%) waliopata alama 0 hadi 1.5 walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi. Wengine waliandika hoja pungufu ya nne huku wengine wakishindwa kujibu kabisa swali hili. Watahiniwa 4,324 (99.3%) waliopata alama sifuri walitoa hoja zisizo sahihi. Watahiniwa hawa hawakuwa na uelewa kuhusu mawazo yaliyotolewa na mwanafalsafa Paulo Freire kuhusiana na jinsi elimu inavyoweza kutumika kama chombo cha ukandamizaji. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza sifa za mfumo rasmi wa elimu kama vile *ina muda maalumu wa mafunzo kwa hiyo elimu inampangia mtu muda wa mafunzo*, *ina ubaguzi wakati wa utoaji wa vyeti, lazima ulipie,* na *haina usawa wa kijinsia*. Mtahiniwa mwingine alieleza kuhusu sifa za elimu ya kikoloni kama vile *kuwepo kwa matabaka, kutofautiana kwa mishahara, ukosefu wa ajira,* na *motisha hasi huweza kutokea pale ambapo mtu anasoma bila ya kupata msaada wowote ule kutoka serikalini mfano upungufu wa ada*. Aidha, mtahiniwa mwingine alitoa hoja zisizo sahihi kama vile *hubagua wanaojua kusoma na wasiojua kusoma, hukandamiza baadhi ya mila na desturi za jamii, hutoa fursa za wasomi katika shughuli mbalimbali,* na *huhitaji gharama*. Majibu haya ya watahiniwa yanathibitisha kuwa hawakuelewa matakwa ya swali. Kielelezo Na. 7.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.


7

(i) Wasomi kutumia taaluma yao katika kutoa rushwa katika mambo ya kiuchumi na kisiasa na kielimu

(ii) ~~Kuch~~ Wasomi kutumia rasilimali za serikali kama za kwao na wengine kushindwa kupata haki zao

(iii) Wasiosoma kunyanyapaliwa kutokana na kukosa maarifa hii kutoka kwa wasomi.


(iv) Wasomi kushindwa kutekeleza majukumu yao mfano walimu na kusababisha kuwakandamiza wanafunzi

**Kielelezo Na. 7.1:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 7.

Katika Kielelezo Na. 7.1, mtahiniwa alitoa hoja zinazohusiana na wasomi kutowajibika ipasavyo katika majukumu yao badala ya kueleza namna elimu inavyoweza kutumika kama chombo cha ukandamizaji kama ilivyoelezwa na mwanafalsafa Paulo Freire.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 11 (0.3%) waliopata alama 3 hadi 4 walitoa hoja sahihi tatu hadi nne kuhusiana na namna ambavyo elimu inaweza kutumika kama chombo cha ukandamizaji kama ilivyoelezwa na Paulo Freire. Watahiniwa 5

(0.1%) waliopata alama zote nne walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mawazo ya mwanafalsafa Paulo Freire katika elimu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja zote sahihi kama vile *mwalimu ndiye mwenye ujuzi na mwanafunzi hupokea tu, mwalimu ndiye mwenye maarifa na mwanafunzi hukariri, mwalimu ndiye msemaji mkuu na mwanafunzi ni msikilizaji tu,* na *mwalimu ndiye anayeongoza na kutoa maadili*. Kielelezo Na. 7.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.


7 (i) Walimu ndio wasemaji wakuu na mwanafunzi husikilize tu.
(ii) Mwalimu ndiye anaefundisha na mwanafunzi hufuata.
(iii) Mwalimu ndiye hutoa kanuni na maadili na mwanafunzi hufuata.
(iv) Mwalimu ndiye chanzo cha maarifa na mwanafunzi hupokea.


**Kielelezo Na. 7.2:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 7.

Aidha, watahiniwa 5 (0.1%) waliopata alama 2 hadi 2.5 walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi, walirudia hoja, na wengine kutoa hoja dhaifu zisizostahili kupata alama zote. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja sahihi kama vile *mwalimu ndiye anayefikiri wanafunzi hukariri* na *mwalimu ndiye msemaji mkuu na wanafunzi wasikilizaji au wapokeaji*. Aidha, alitoa hoja zisizo sahihi kama vile *elimu hulenga nadharia bila vitendo* na *elimu inayotolewa haikidhi mahitaji ya jamii*. Mtahiniwa mwingine alitoa hoja sahihi kama vile *mwalimu ndiye chanzo cha maarifa* na *wanafunzi hufanywa benki ya kuhifadhia maarifa yanayotoka kwa mwalimu.* Aidha, alitoa hoja zisizo sahihi kama vile *watu masikini hawawezi kujiinua kiuchumi bila matajiri* na *elimu inayotolewa haimpi mwanafunzi mwanga.* Majibu hayo yanaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya namna ambavyo elimu inaweza kutumika kama chombo cha ukandamizaji kama ilivyoelezwa na mwanafalsafa Paulo Freire.

### 2.1.8 Swali la 8: Upimaji katika Elimu

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kueleza kwa ufupi misingi minne ya kufuata katika upangaji wa maswali ya mtihani. Jumla ya watahiniwa 4,354 (100%) walijibu swali hili. Takwimu za ufaulu wa watahiniwa katika swali hili zinaonesha kuwa watahiniwa 2,025 (46.5%) walipata alama 0 hadi 1.5, watahiniwa 1,480 (34%)

walipata alama 2 hadi 2.5, na watahiniwa 849 (19.5%) walipata alama 3 hadi 4. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 8.





**Chati Na. 8:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 8*

Chati Na. 8 inaonesha kuwa asilimia 46.5 ya watahiniwa walipata alama 0 hadi 1.5, asilimia 34 walipata alama 2 hadi 2.5, na asilimia 19.5 walipata alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu wa wastani kwa kuwa asilimia 53.5 ya watahiniwa walipata alama 2 hadi 4.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 2,025 (46.3%) waliopata alama 0 hadi 1.5 walikuwa na maarifa kidogo kuhusu dhana ya upangaji wa maswali ya mtihani. Watahiniwa hao walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi na wengine walitoa hoja dhaifu. Watahiniwa 614 (14.1%) walipata alama sifuri kwa sababu hawakuwa na maarifa katika kipengele cha utungaji wa majaribio na mitihani. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza misingi ya upangaji maswali kama vile *idadi ya wanafunzi, maswali yawe ya kufikirisha, jina la mtihani,* na *maswali yawe ni ya kupima ufahamu wa mwanafunzi.* Mtahiniwa mwingine alitoa hoja zisizo sahihi kama vile *kupanga maswali ya kuchagua jibu sahihi, kupanga maswali ya kuoanisha yaani A na B, kupanga maswali ya kujibu nafasi zilizo achwa wazi,* na *kuandika maswali ya kweli au si kweli*. Pia, mtahiniwa mwingine alitoa hoja sizizo sahihi kama vile *maswali yawe yanapima ufahamu wa mwanafunzi, maswali yasiwe ya kupotosha wanafunzi, maswali yawe yanapima ujuzi alionao mwanafunzi,* na *maswali yasiwe chini ya asilimia 24 na yasiwe juu ya asilimia 85.* Majibu haya yanaonesha kuwa watahiniwa hawa hawakuwa na

maarifa kuhusu mambo muhimu ya kuzingatia katika upangaji wa maswali ya mtihani. Kielelezo Na. 8.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.



8

a) kuwaeleza maana ya Upangaji wa maswali ya mtihani

b) Kuwaeleza faida za Upangaji wa maswali ya mtihani

c) Kuwaeleza Umuhimu ~~unao~~ wa Upangaji wa maswali ya mtihani.

d) Pia na mambo yanayotakiwa kuzingatiwa wakati wa upangaji wa mtihani.


**Kielelezo Na. 8.1:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 8.

Katika Kielelezo Na. 8.1, mtahiniwa aliandika namna atakavyowafundisha wanafunzi mada ya upangaji wa maswali badala ya kuandika misingi ya kufuata katika upangaji wa maswali ya mtihani.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 1,480 (34%) waliopata alama 2 hadi 2.5 walikuwa na mapungufu mbalimbali katika majibu yao kama vile kuchanganya hoja sahihi na zisizo sahihi, kurudia hoja na kutoa hoja pungufu au dhaifu zisizostahili kupata alama zote. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja sahihi kama vile *kupanga maswali mepesi kwenda magumu* na *kuanza na maswali ya majibu mafupi kwenda majibu marefu.* Pia, alitoa hoja zisizo sahihi kama vile *maswali yawe ya kumfikirisha mwanafunzi* na *maswali yapangwe kulingana na ngazi za mada zilivyo*. Mtahiniwa mwingine alitoa hoja sahihi kama vile *maswali yatoke kwenye mada zilizofundishwa* na *yapangwe kwa kuanzia na yaliyo rahisi na kumalizia na yaliyo magumu*. Pia, mtahiniwa huyu alitoa hoja zisizo sahihi kama vile *jina la mtihani* na *kuzingatia kiwango cha mlengwa*. Majibu haya yanaonesha kuwa watahiniwa katika kundi hili walikuwa na maarifa ya wastani juu ya misingi ya kufuata katika upangaji wa maswali ya mtihani.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 849 (19.5%) waliopata alama 3 hadi 4 walieleza kwa usahihi misingi minne ya kufuata katika upangaji wa maswali ya mtihani. Watahiniwa 300 (6.9%) waliopata alama zote nne walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana nzima ya utungaji wa majaribio na mitihani. Baadhi ya hoja sahihi zilizotolewa na mtahiniwa mmojawapo ni kama vile *kuzingatia mada zilizofundishwa katika kipindi husika, kuzingatia aina ya maswali yatakayotumika katika mtihani, kuzingatia idadi ya*


*maswali katika kila mada zilizofundishwa,* na *kuzingatia alama ya kila swali katika kila kipengele.* Kielelezo Na. 8.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.


8 Yafuatayo ni mambo ya kuzingatia katika -
upangaji wa maswali katika mtihani.
i) Kupanga maswali marahisi kuelekea maswali
magumu ili kuweza kutoa motisha kwa mwa
nafunzi kuweza kuendelea kufanya maswali
mengine.
ii) Kuandika maelekezo ya mtihani yanayo elewe
ka kwa mtahiniwa.
iii) Kupanga maswali katika sehemu zenye
mgawanyo mzuri mfano sehemu A" masw
ali yanayohitaji jibu moja fupi na B", C".
iv) Kurudia kusoma maelekezo katika ~~upan~~
mtihani uliyoandika ili kuweza kuba
ini makosa.

**Kielelezo Na. 8.2:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 8.

### 2.1.9 Swali la 9: Mtaala


Swali hili lilimtaka mtahiniwa kutoa hoja nne za kuzingatia katika kuhariri vitabu vya kiongozi cha mwalimu. Jumla ya watahiniwa 4,354 (100%) walijibu swali hili. Takwimu za ufaulu wa watahiniwa katika swali hili zinaonesha kuwa watahiniwa 48 (1.1%) walipata alama 0 hadi 1.5, watahiniwa 205 (4.7%) walipata alama 2 hadi 2.5, na watahiniwa 4,101 (94.2%) walipata alama 3 hadi 4. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 9.




**Chati Na. 9**: *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 9*

Chati Na. 9 inaonesha kuwa asilimia 1.1 ya watahiniwa walipata alama 0 hadi 1.5, asilimia 4.7 walipata alama 2 hadi 2.5, na asilimia 94.2 walipata alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa asilimia 98.9 ya watahiniwa walipata alama 2 hadi 4.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 4,101 (94.2%) waliopata alama 3 hadi 4 walieleza kwa usahihi hoja nne za kuzingatia katika kuhariri vitabu vya kiongozi cha mwalimu. Watahiniwa 3,118 (71.6%) waliopata alama zote nne walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu sifa ya kitabu cha kiongozi cha mwalimu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza hoja sahihi kama vile *kiwe na mada zote zilizopo katika muhtasari, kioneshe mbinu na njia za kufundishia na kujifunzia, kioneshe malengo mahususi ya mada husika,* na *kiwe na majibu ya mazoezi yote yaliyopo kwenye kitabu cha kiada*. Pia, mtahiniwa mwingine aliyejibu swali hili kwa usahihi aliandika hoja kama vile *kiwe na mada zilizopo kwenye muhtasari na kitabu cha kiada, kinatakiwa kioneshe njia na mbinu za kufundishia na kujifunzia, kiwe na majibu yote ya maswali yaliyopo kwenye kitabu cha kiada,* na *kioneshe vifaa au zana ambazo mwalimu anatakiwa kuzitumia katika mada husika.* Majibu haya ya watahiniwa yanaonesha kuwa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mambo ya kuzingatia katika kuhariri vitabu vya kiongozi cha mwalimu. Kielelezo Na. 9.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.



9 i) Kionesha mada/maudhui/umahiri wa kwenye kitabu cha kiada.

ii) Kionesha majibu ya mazoezi ya kwenye kitabu cha kiada.


iii) Kionesha mbinu/njia zitakazotumika katika ufundishaji.

iv) Kionesha zana/vifaa vya kufundishia.

**Kielelezo Na. 9.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 9.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 205 (4.7%) waliopata alama 2 hadi 2.5 walieleza hoja dhaifu na wengine kuchanganya hoja sahihi na zisizo sahihi, hivyo, kupata alama za wastani. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza hoja sahihi kuhusu kiongozi cha mwalimu kama vile *lazima kiwe kinaonesha zana na hatua za ufundishaji na ujifunzaji* na *lazima kiwe na majibu ya maswali yaliyomo katika kitabu cha kiada.* Aidha, alitoa hoja mbili zisizo sahihi ambazo ni *lazima kiwe kidogo* na *lazima kiwe na jarada gumu*. Mtahiniwa mwingine katika kundi hili alieleza sifa kama vile *lazima kiwe kina majibu ya maswali, kiwe kinaonesha mbinu mbalimbali zinazomwongoza mwalimu katika ufundishaji, kiwe kina cheti cha ithibaki cha Taasisi ya Elimu Tanzania* na *kiwe kina ganda gumu*. Katika majibu yake, hoja ya tatu na ya nne hazikuwa sahihi. Hivyo, alipata alama za wastani. Majibu hayo yanaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya sifa za kitabu cha kiongozi cha mwalimu.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 48 (1.1%) waliopata alama 0 hadi 1.5 walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi na wengine walitoa hoja pungufu. Aidha, watahiniwa wengine walitoa hoja zenye kujirudia au kutoa hoja dhaifu hivyo, kupata alama za chini ya wastani. Watahiniwa 12 (0.3%) walipata alama sifuri kwa sababu hawakuwa na maarifa kuhusu sifa za kiongozi cha mwalimu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliyepata alama moja alieleza kuwa: *kiwe na haki thibati, jina la mwandishi au mchapishaji,* na *mwaka wa kuchapishwa*. Aidha, aliandika jibu moja sahihi ambalo ni *kiwe na zana, njia na majibu ya kitabu cha kiada.* Mtahiniwa mwingine alieleza hoja zisizo sahihi kama vile *kiwe kina mwonekano mzuri wa ndani na nje, kiwe kinaendana na walimu, vilevile, kisiwe na karatasi nyingi,* na *kiwe na jalada gumu.* Majibu haya yanaonesha kuwa watahiniwa katika kundi hili hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusiana na mambo ya kuzingatia katika kuhariri vitabu vya kiongozi cha mwalimu. Kielelezo Na. 9.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye hakuelewa matakwa ya swali na hakuwa na maarifa ya kutosha.




| 9 | Sifa 20 kiongozi cho Mwalimu anazopaswa |
| --- | --- |
| | kuzingatia wakati wa kutekeleza kazi |
| | i) Awe Mwalimu Mahiri |
| | ii) Awe mwalimu ambaye anajivunia wa |
| | kufanya kazi hiyo |
| | iii) Awe mwalimu mzoefu wa hiyo kazi. |
| | iv) Awe mwalimu anayeweza kufundisha vizuri |
| | hii hilo |

**Kielelezo Na. 9.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 9.

Katika Kielelezo Na. 9.2, mtahiniwa alieleza sifa za mwalimu mzuri badala ya sifa za kitabu cha kiongozi cha mwalimu.

### 2.1.10 Swali la 10: Uongozi wa Elimu Tanzania


Swali hili lilimtaka mtahiniwa kueleza kwa ufupi majukumu manne ya Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi. Jumla ya watahiniwa 4,354 (100%) walijibu swali hili. Takwimu za ufaulu wa watahiniwa katika swali hili zinaonesha kuwa watahiniwa 7 (0.2%) walipata alama 0 hadi 1.5, watahiniwa 6 (0.1%) walipata alama 2 hadi 2.5, na watahiniwa 4,341 (99.7%) walipata alama 3 hadi 4. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 10.




**Chati Na. 10:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 10*

Chati Na. 10 inaonesha kuwa asilimia 0.2 ya watahiniwa walipata alama 0 hadi 1.5, asilimia 0.1 walipata alama 2 hadi 2.5, na asilimia 99.7 walipata alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kuliko maswali mengine kwa kuwa asilimia 99.8 ya watahiniwa walipata alama 2 hadi 4.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 4,341 (99.7%) waliopata alama 3 hadi 4 walielewa matakwa ya swali na walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Uongozi wa Elimu Tanzania hasa majukumu ya Mwalimu Mkuu katika Shule za Msingi. Vilevile, walitoa hoja sahihi tatu hadi nne zilizoelezea majukumu ya Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi. Watahiniwa 4,259 (97.8%) waliopata alama zote nne walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu majukumu ya Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi. Hivyo, walitoa hoja nne sahihi. Mtahiniwa mmojawapo alieleza majukumu sahihi ya Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi kama vile *kuratibu na kusimamia shughuli zote zinazofanyika shuleni, kukagua walimu mara kwa mara utendaji wao wa kazi katika ufundishaji, kuwaandikisha wanafunzi wa darasa la awali na la kwanzo shuleni,* na *kuunganisha uhusiano wa shule na jamii inayoizunguka shule*. Majibu ya watahiniwa katika kundi hili yanaonesha kuwa pamoja na maarifa waliyoyapata wakati wa ufundishaji na ujifunzaji, uzoefu walioupata wakati wa mazoezi ya kufundisha vimewasaidia kujua vyema majukumu ya Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi. Kielelezo Na. 10.1 ni sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali hili.


10

i) Kusimamia Walimu katika utendaji kazi mfano, mwalimu kuingia darasani kwa wakati na kuwa na vifaa vya kufundishia kama Andalio, Azimio na nukuu.

ii) Kusimamia nidhamu ya walimu kazini mfano kuwahi kazini, na kutofanya mambo kinyume cha sheria iliyopangwa.


iii) Kusimamia mahudhurio ya wanafunzi shuleni na kutoa adhabu kwa wanafunzi.

iv) Kusimamia maendeleo ya wanafunzi pamoja na walimu shuleni, mfano kujua matatizo yanayowakumba katika ufundishaji na ujifunzaji.

**Kielelezo Na. 10.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 10.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa ulibaini kuwa watahiniwa 7 (0.2%) waliopata alama 0 hadi 1.5 hawakuwa na maarifa ya kutosha katika dhana ya uongozi bora wa shule. Hivyo, waliandika hoja zisizostahili na wengine kuandika

hoja pungufu ya nne na kupata alama za chini. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliyepata alama moja aliandika hoja moja sahihi ambayo ni *kuwasimamia walimu katika kuwahi kazini.* Kielelezo Na. 10.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.



| 10 | |
|---|---|
| i. | KUANDAA AZIMIO LA KAZI |
| ii | KUANDAA ANDALIO LA SOMO |
| iii | KUANDAA SHAJARA YA SOMO |
| iv | KUANDAA NUKUU ZA SOMO. |

**Kielelezo Na. 10.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 10.

Katika Kielelezo Na. 10.2, mtahiniwa aliorodhesha kazi anazopaswa kuzifanya mwalimu hasa juu ya maandalizi ya nyaraka muhimu kabla ya kuingia darasani badala ya kueleza majukumu ya Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 6 (0.1%) waliopata alama 2 hadi 2.5 walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi na wengine kutoa hoja dhaifu hivyo, kupata alama za wastani. Kwa mfano, mtahiniwa mmojawapo alitoa hoja mbili sahihi ambazo ni *kufuatilia utendaji kazi wa walimu* na *kufuatilia maendeleo ya taaluma katika shule*. Aidha, mtahiniwa huyo alitoa hoja zisizo sahihi kama vile *mwenyekiti wa kamati ya shule* na *mwenyekiti wa kamati ya ujenzi ya shule*. Majibu hayo yanaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu majukumu ya Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi.


## 2.2 SEHEMU B: Maswali ya Insha

Maswali katika sehemu B yalitoka katika mada nne (4) ambazo ni *Makuzi na Ukuaji wa Mtoto, Mtaala, Upimaji katika Elimu* na *Taaluma ya Ualimu*. Kila swali lilikuwa na alama 15, hivyo, kufanya jumla ya alama sitini (60) katika sehemu hii.

### 2.2.1 Swali la 11: Makuzi na Ukuaji wa Mtoto

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kutumia hoja sita kuonesha mchango wa sifa zilizorithiwa kwenye haiba ya mtoto. Jumla ya watahiniwa 4,354 (100%) walijibu swali hili. Takwimu za ufaulu wa watahiniwa katika swali hili zinaonesha kuwa watahiniwa 3,211 (73.7%) walipata alama 0 hadi 5.5, watahiniwa 1,020 (23.5%) walipata alama 6 hadi 10, na watahiniwa 123 (2.8) walipata alama 10.5 hadi 14.

Hakukuwa na watahiniwa waliopata alama zote 15. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na.11.




**Chati Na. 11:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 11*

Chati Na. 11 inaonesha kuwa asilimia 73.7 ya watahiniwa walipata alama 0 hadi 5.5, asilimia 23.5 walipata alama 6 hadi 10, na asilimia 2.8 walipata alama 10.5 hadi 14. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa hafifu kwa kuwa asilimia 26.3 ya watahiniwa ndio waliopata alama 6 hadi 14.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 3,211 (73.7%) waliopata alama 0 hadi 5.5 hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu namna ambavyo sifa zilizorithiwa zinaweza kuchangia haiba ya mtoto. Hivyo, walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi na wengine kushindwa kuelezea hoja ambazo zilikuwa ni sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmojawapo aliyepata sifuri alielezea hoja zisizo sahihi kama vile *mazingira, jamii, mila na desturi,* na *utamaduni*. Pia, mtahiniwa mwingine aliyepata alama sifuri alitoa hoja zisizo sahihi kama vile *balehe, walimu, tamaa, umasikini, makundirika,* na *mazingira*. Mtahiniwa mwingine alichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi. Hoja sahihi alizotoa ni kama vile *upole* na *ugonjwa*. Pia, alitoa hoja zisizo sahihi kama vile *wizi, matumizi mabaya ya lugha,* na *uongeaji kwa sana*. Majibu ya watahiniwa hao yanaonesha kuwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu athari za sifa zilizorithiwa kwenye haiba ya mtoto na wengine walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi hivyo, kupata alama za chini. Kielelezo Na. 11.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kukidhi matakwa katika swali hili.

11

Sifa zilizorithiwa, Ni sifa ambazo mtoto huzipata kutokana na kurithi pengine tabia au mienendo mizima ya kimaisha ka tika ufendaji. Mfano wa sifa zilizorithiwa k ama vile, mila, desturi, maadili mema na ha ta tabia zetu. Hapa tunaelenda kuangali a sifa zilizorithiwa ambazo huchangia h aiba ya mtoto. Yafuatayo ni mafokeo ya si fa zilizorithiwa kuweza kuchangia haiba ya mtoto.

Humsaidia mtoto kutunza tamaduni; mfano, uvaaji na shughuli nzima za ki la siku katika jamii anayoishi na kuw eza kufuata utamaduni kutokana na sifa alizorithi.

Humwezesha kuishi na watu vizu uri kwenye jamii; hii kutokana na sifa alizorithi ambazo zina maadili maazuri na mafunzo, hivyo humsaidia kuweza kuishi na watu mbalimbali.

Humjengea maadili mema mtoto; mfano, kuamkia wakubwa na kuheshimu w aliomzidi umri, hivyo yote hayo hutoka na na sifa zilizorithiwa kwa mtoto kupitia wazazi au ndugu.

Humjengea upendo katika kuishi na watu; mfano, kujali, kuthamini, hii ni kutokana na sifa zilizorithiwa kutoka kwa wazazi au familia ambayo anato ka au jamii fulani kutokana na ma lezi aliyopata.

11 Cont.

Humjengea mtoto ushirikiano s aidi na wengine; katika jamii na mambo mbalimbali yanayotokea katika taifa lake na uzalendo.

Humfanya mtoto kuwa na mip aka katika ufendaji wa jambo; hii huzing atia sika na uwepo wa watu wazima hivyo huweza kuwa na mipaka na kuh eshimu watu mbalimbali.

Hivyo basi; sifa zilizorithiw a huweza kuchangia haiba ya mtoto k wa kumsaidia mtoto kutunza tamad uni zao na hata kuweza kuishi na watu vizuri kwenye jamii.

**Kielelezo Na. 11.1:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 11.

Katika Kielelezo Na. 11.1, mtahiniwa alieleza faida ya sifa zisizo za kurithi kwenye haiba ya mtoto badala ya kueleza athari ya sifa zilizorithiwa kwenye haiba ya mtoto.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa 1,020 (23.5%) waliopata alama 6 hadi 10 walikuwa na maarifa ya wastani kuhusu athari ya sifa zilizorithiwa kwenye haiba ya mtoto. Katika insha zao walionesha kuwa na mapungufu mbalimbali kama vile utangulizi usiojitosheleza, kutoa hoja pungufu, kutoa hitimisho lisiloendana na matakwa ya swali, kushindwa kutetea hoja, kuchanganya hoja sahihi na zisizo sahihi hivyo, kupelekea kupata alama za wastani. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja sahihi kama vile *upole, magonjwa,* na *unene.* Aidha, alitoa hoja zisizo sahihi kama vile *uvumilivu, wizi,* na *uongo*. Pia, mtahiniwa mwingine alitoa hoja sahihi kama vile *ucheshi, ukali, urefu na ufupi,* na *upole* lakini alishindwa kuzielezea kwa ufasaha. Aidha, alitoa hoja mbili zisizo sahihi ambazo ni *wizi* na *uvumilivu.* Majibu hayo yanaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu athari ya sifa zilizorithiwa kwenye haiba ya mtoto.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 123 (2.8%) waliopata alama 10.5 hadi 14 walionesha kwa usahihi athari ya sifa zilizorithhiwa kwenye haiba ya mtoto. Watahiniwa 5 (0.1%) waliopata alama 14 walidhihirisha kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu athari ya sifa zilizorithiwa kwenye haiba ya mtoto. Walianza na utangulizi uliojitosheleza na maelezo sahihi ya kutetea hoja zao. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja sahihi kama vile *uzuri wa sura, akili nyingi au duni, upole au ucheshi, rangi nyeupe au nyeusi, maumbile,* na *magonjwa mbalimbali*. Mtahiniwa mwingine alielezea hoja sahihi kama vile *rangi nyeupe au nyeusi, maumbile ya unene au kawaida, akili, magonjwa,* na *upole*. Kielelezo Na. 11.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.

11

Haiba, ni mambo yote yanayomtofautisha, au kumfananisha mtu mmoja na mtu mwingine, haiba inaweza ikarithiwa kutoka kwa wazazi lakini pia haiba inaweza ikarithiwa kutokana na mazingira anayoishi mtoto, zifuatazo ni mambo yanayorithiwa ambayo yanaweza kuchangia haiba ya mtoto.

Magonjwa, mfano UKIMWI, mtoto akirithi magonjwa kutoka kwa wazazi wake kunaweza kumjengea haiba ya kujiona yeye ni mpweke na mnyonge kila wakati.

Maumbile, mtoto akirithi maumbile makubwa (unene) kutoka kwa wazazi wake anaweza ~~akajiona yeye ni~~ kumjengea haiba ya ubabe kwa wanafunzi au watoto wenzie anaocheza nao na kusoma nao.

Uwezo wa akili, pia mtoto anaweza kuji~~ona yeye ad~~vuna na kujiona yeye anaweza kila kila akirithi uwezo wa akili mkubwa kutoka wa wazazi wake.

Uzuri, mtoto akirithi uzuri kutoka kwa wazazi wake kunaweza kumjengea haiba ya kujivuna na kujisikia kwa wenzie na kuona wenzie si lolote si chochote.

Tabia, pia mtoto ~~akirit~~ anaweza akarithi tabia za wazazi wake mfano upole, unyenyekevu, subira, mtoto akirithi tabia hizi ~~kwa~~ humjengea haiba ya upole na unyenyekevu kwa watu wengine.

Ulemavu wa ngozi (Albino), mwanafunzi akiwa na ulemavu wa ngozi (Albino) mara

11 Cont.

nyingi ~~kujio~~ hujitenga na wenza~~ke~~ katika shughuli za ujifunzaji na ~~vitendo~~ shughuli zingine hii huweza kumjengea haiba ya unyonge kila wakati.


Kwahiyo, Baadhi ya haiba ya mtoto hujengwa kutokana na kurithi baadhi ya vitu kutoka kwa wazazi wake.

**Kielelezo Na. 11.2:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 11.

### 2.2.2 Swali la 12: Mtaala

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kuchambua vipengele sita vya mtaala ambavyo huwawezesha walimu kujua majukumu yao katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Jumla ya watahiniwa 4,354 (100%) walijibu swali hili. Takwimu za

ufaulu wa watahiniwa katika swali hili zinaonesha kuwa watahiniwa 1,415 (32.5%) walipata alama 0 hadi 5.5, watahiniwa 1,779 (40.9%) walipata alama 6 hadi 10, na watahiniwa 1,160 (26.6%) walipata alama 10.5 hadi 14.5. Hakuna watahiniwa waliopata alama zote 15. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 12.




**Chati Na. 12:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 12*

Chati Na. 12 inaonesha kuwa asilimia 32.5 ya watahiniwa walipata alama 0 hadi 5.5, asilimia 40.9 walipata alama 6 hadi 10, na asilimia 26.6 walipata alama 10.5 hadi 14.5. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu wa wastani kwa kuwa asilimia 67.5 ya watahiniwa walipata alama 6 hadi 14.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 1,779 (40.9%) waliopata alama 6 hadi 10 walishindwa kutoa maelezo sahihi katika hoja zao. Pia, wapo watahiniwa ambao walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi na wengine kutoa hoja dhaifu hivyo, kupata alama pungufu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alichambua vipengele vya mtaala kuwa ni *muda wa mafunzo, majukumu ya mwalimu, idadi ya vipindi, njia za kufundishia na kujifunzia, vifaa au zana za kufundishia na kujifunzia,* na *umahiri mkuu.* Mtahiniwa huyu katika hoja ya kwanza na ya mwisho alichambua vipengele ambavyo siyo sehemu ya vipengele vya mtaala. Aidha, katika vipengele sahihi vya mtaala, mtahiniwa huyo hakutoa maelezo yaliyojitosheleza hivyo, alipata alama za wastani. Mtahiniwa mwingine alichambua vipengele vya mtaala kuwa ni *mbinu za kufundishia na kujifunzia, zana za kufundishia na kujifunzia,* na *zana za upimaji wa maendeleo ya wanafunzi*. Pia, alielezea vipengele ambavyo siyo sahihi kama vile *falsafa ya elimu, mahitaji ya jamii,* na *falsafa ya nchi*. Hivyo, mtahiniwa huyu alipata alama za wastani

kutokana na kuchanganya hoja sahihi na zisizo sahihi. Majibu hayo ya watahiniwa yanaonesha kuwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusiana na vipengele vya mtaala.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 1,415 (32.5%) waliopata alama 0 hadi 5.5 walikuwa na uelewa mdogo kuhusu vipengele vya mtaala ambavyo vinamwezesha mwalimu kujua majukumu yake katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Hivyo, walitoa hoja zisizo sahihi. Watahiniwa 34 (0.8%) waliopata alama sifuri hawakuelewa matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alichambua vipengele vya mtaala visivyo sahihi ambavyo ni *muhtasari wa somo, azimio la kazi, andalio la somo, shajara la somo, vitabu vya kiada na ziada,* na *kiongozi cha mwalimu*. Mtahiniwa huyu alichambua vifaa vya mtaala badala ya vipengele vya mtaala. Vilevile, mtahiniwa mwingine alichambua vipengele vya mtaala visivyo sahihi kama vile *muhtasari, kiongozi cha mwalimu, kitabu cha mwanafunzi, mahitaji ya jamii, sera ya nchi,* na *falsa ya nchi*. Kimsingi, watahiniwa hawa walitakiwa kuchambua vipengele vya mtaala ambavyo ni *utangulizi, malengo ya mtaala, muda wa mafunzo, lugha ya kufundishia na kujifunzia, masomo yatakayotolewa, idadi ya vipindi, njia za kufundishia na kujifunzia, vifaa au zana za kufundishia na kujifunzia,* na *upimaji wa maendeleo ya wanafunzi*. Kielelezo Na. 12.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali la 12 kwa usahihi.

| 12 | |
|---|---|
| | Vipengele Vya Mtaala |
| | Mtaala; Mambo yote yaliyopangwa na Siasa, jamii, wadau Mbalimbali wa elimu, Vyuo vya Ushirika katika kuendeleza Elimu. Kuna aina tatu ya Mtaala, Mtaala Rasmi, Mtaala Usiorasmi na Mtaala Mficho |
| | Ufuatazo ni Vipengele vya Mtaala zinazomwezesha Mwalimu kujua Majukumu ya Ufundishaji na Ujifunzaji. |
| | Muhtasari; Ni mambo au Utaratibu Unaoeleza kwa kifupi mambo yote yanayofundishwa kwa wiki, Mwezi, Muhula au Mwaka Mzima, Muhtasari huonesha Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi pia huonesha Zana na Mbinu Zitakazotumika katika Ufundishaji na Ujifunzaji |
| | Azimio la kazi; ni kanuni au Utaratibu au mpango Ulioandaliwa na Mwalimu kwa kufuata Muhtasari kwa kuanza na Mada rahisi kumalizia mada ngumi ili kurahisisha Shughuli za Ufundishaji na Uji-funzaji |
| | Kitabu cha kiada ni kitabu kinachotumiwa na Mwalimu pamoja na Mwanafunzi katika kufanya Marudio ya kujisomea ili aweze kupata Maarifa na Ujuzi Uliobora Zaidi |
| | Kitabu cha Ziada ni kile kitabu kinachotumiwa na Mwanafunzi ili kujipatia Maarifa ya ziada kwa kusoma maswali na Mazoezi yaliyo katika kitabu hicho cha Ziada |
| | Rejea; Rejea ni Moja ya kipengele cha Mtaala na imepitishwa katika Taasisi ya elimu Tanzania kuwa rejea zitumike katika mchakato mzima wa Ufundishaji na Ujifunzaji ili wanafunzi waweze kujipatia maarifa Mfano wa rejea hizo ni kama Vile Magazeti, Vitini Mbalimbali |

| 12 Cont. | |
|---|---|
| | Kiongozi cha Mwalimu; Ni mwongozo Unaomwongoza Mwalimu katika Suala zima la Ufundishaji kwa kufuata hatua na Mbinu zinazotumika katika Ufundishaji pia na Zana Zitakazotumika katika Ufundishaji |
| | Hivyo basi, Vipengele vya Mtaala ni muhimu Sana katika mchakato wa Ufundishaji na Ujifunzaji kwa sababu bila Vipengele hivyo vya Mtaala huwezi Ukafanya Shughuli hizo za Ufundishaji na Ujifunzaji |

**Kielelezo Na. 12.1:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 12.

Katika Kielelezo Na.12.1, mtahiniwa alichambua vifaa vya mtaala badala ya kuchambua vipengele vya mtaala ambavyo huwawezesha walimu kujua majukumu yao katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 1,160 (26.6%) waliopata alama 10.5 hadi 14.5 walikuwa na uelewa mzuri kuhusu vipengele vya mtaala ambavyo huwawezesha walimu kujua majukumu yao katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Watahiniwa waliopata alama 14 na 14.5 walichambua kwa usahihi vipengele sita vya mtaala hivyo, walipata alama za juu. Kwa mfano, mtahiniwa mmojawapo alichambua kwa usahihi vipengele hivyo kuwa ni *utangulizi, malengo ya mtaala, masomo yatakayofundishwa, lugha ya kufundishia, zana za kufundishia na kujifunzia,* na *kipengele cha idadi ya vipindi.* Katika uchambuzi wa majibu ya watahiniwa inaonesha kuwa maarifa waliyoyapata darasani pamoja na uzoefu walioupata katika mazoezi ya kufundisha wakiwa mwaka wa kwanza na wa pili vimewasaidia kuvijua vyema vipengele vya mtaala vinavyomwezesha mwalimu kujua majukumu yake katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Kielelezo Na. 12.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.

Mtaala ni jumla ya mpango ulioandaliwa na Kuratibiwa kwa lengo la kuwapatia walengwa stadi, maarifa na mielekeo mbalimbali. pia mtaala ndio unaozaa Muhtasari wa somo na walimu wanaopaswa kufundisha mtaala ni wale waliofuzu grade "A" cheti. Zifuatazo ni vipengele vya mtaala ambavyo huwawezesha walimu kufua majukumu yao katika michakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

Utangulizi, Ni mojawapo ya vipengele vya mtaala kwani katika utangulizi ndio huonesha sababu za kuandaliwa kwa mtaala huo. Hivyo basi kipengele hiki huwawezesha ~~wana~~ walimu kufua majukumu yao kwani katika utangulizi mwalimu huweza kubaini ~~[illegible]~~ anavyopaswa kufundisha

Malengo, Mtaala unapoandaliwa huwa na malengo ambayo huwawezesha walengwa kupata stadi na mielekeo mbalimbali. Hivyo kipengele hiki huwasaidia walimu wanapofundisha kufua ni malengo gani mwanafunzi anapaswa kupata baada ya kujifunza mada husika. Hivyo basi Malengo ya mtaala ni vipengele mojawapo ambayo huwawezesha walimu kufua majukumu yao.

Masomo yatakayofundishwa, Hii pia ni kipengele cha mtaala kwani huonesha masomo yanayopaswa kufundishwa mashuleni mfano Uraia, Sayansi Hisabati, English na mengineyo. Huwasaidia walimu kuweza kufua majukumu yao kwani kila mwalimu atafundisha somo analolielewa na hii ni kutokana na Mtaala kuainisha masomo yanayopaswa kufundishwa katika ngazi fulani ya elimu

Lugha ya kufundishia na kujifunzia. Mtaala unapoandaliwa huonyesha lugha ipi inapaswa kufundi


| 12 Cont. | |
|---|---|
| | shia ngazi fulani ya elimu mfano katika shule za msingi lugha ya kufundishia ni kiswahili isipokuwa katika somo la Kingereza lakini katika shule za sekondari lugha ya kufundishia huwa ni Kingereza kwa masomo yote isipokuwa kiswahili. Hivyo inakuwa rahisi kwa mwalimu kuweza kutambua majukumu yake katika ufundishaji na ujifunzaji kwani hawezi akatumia lugha ya kingereza katika shule za msingi kufundishia masomo yote na hii ni kutokana na mtaala kuonyesha lugha zinazopaswa kufundishia na kujifunzia mashuleni. |
| | Muda wa Mafunzo, Mtaala unapoandaliwa huonyesha muda wa kumaliza mafunzo mfano kwa mwaka au miaka. Hivyo inakuwa rahisi kwa mwalimu wakati wa utekelezaji wa majukumu yake kwani kipengele hiki cha mtaala kitamsaidia kubaini kuwa baada ya majuma au miezi awe amekamilisha anachotakiwa kufundisha ili muda wa mafunzo wa mtaala huo usikute bado hajamaliza. Hivyo basi Muda wa mafunzo huwasaidia au huwawezesha walimu kujua majukumu yao katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji |
| | Zana au vifaa vya kufundishia na kujifunzia, kipengele hiki huwasaidia walimu kujua majukumu yao katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji kwani huwezesha mwalimu kuweza kubaini zana anazotakiwa kutumia ili kukamilisha tendo la ufundishaji mfano vitu halisi, michoro, picha, ramani na vielelezo mbalimbali, hivyo inakuwa rahisi kwa mwalimu kuandaa zana hizo. |
| | Hivyo basi mtaala pia una umuhimu wake katika kujifunza kwani huweza kudhibiti mfumo wa elimu na hii ni ili kila shule kutokuwa na mtaala wake, kuwaongoza walimu wasitoke nje ya malengo makuu ya somo |

| 12 Cont. | |
|---|---|
| | na falsafa ya nchi pia husaidia kurekebisha na kuendeleza elimu kupitia watafiti mbalimbali. Wadau wa kielimu pia mtaala huweza kuwasaidia walimu na wanafunzi kujua madhumuni ya elimu. |

**Kielelezo Na. 12.2:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 12.

### 2.2.3 Swali la 13: Upimaji katika Elimu

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kufafanua manufaa matatu na mapungufu matatu ya maswali ya kuchagua jibu sahihi. Jumla ya watahiniwa 4,354 (100%) walijibu swali hili. Takwimu za ufaulu wa watahiniwa katika swali hili zinaonesha kuwa watahiniwa 636 (14.6%) walipata alama 0 hadi 5.5, watahiniwa 2,155 (49.5%) walipata alama 6 hadi 10, na watahiniwa 1,563 (35.9%) walipata alama 10.5 hadi 15. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 13.




**Chati Na. 13:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 13*

Chati Na. 13 inaonesha kuwa asilimia 14.6 ya watahiniwa walipata alama 0 hadi 5.5, asilimia 49.5 walipata alama 6 hadi 10, na asilimia 35.9 walipata alama 10.5 hadi 15. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa asilimia 85.4 ya watahiniwa walipata alama 6 hadi 15.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 2,155 (49.5%) waliopata alama 6 hadi 10 walitoa utangulizi sahihi ingawa walishindwa kuchambua vizuri hoja zao. Wengine walitoa hoja zisizo sahihi hivyo, walipata alama za wastani. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja sahihi kwa upande wa faida kama vile *kurahisisha usahihishaji, kupima maarifa mengi kwa muda mfupi,* na *huokoa muda.* Vilevile, alitoa hoja zisizo sahihi kwa upande wa mapungufu kama vile *haimjengei kumbukumbu za kudumu mwanafunzi,* na *mwanafunzi anaweza kuchagua jibu lisilo sahihi.* Aidha, mtahiniwa huyu alitoa hoja moja sahihi kwa upande wa mapungufu ya maswali ya kuchagua jibu sahihi ambayo ni *haimjengei mwanafunzi udadisi.* Pia, mtahiniwa mwingine alitoa faida kama vile *hutumia muda mchache kujibu maswali hayo* na *ni rahisi kuyasahihisha*. Vilevile,

alitoa hoja isiyo sahihi kwa upande wa faida ambayo ni *rahisi kuyaandaa*. Kwa upande mwingine, alieleza mapungufu ya maswali hayo kuwa ni *hayapimi ujuzi wa kujieleza* na *mwanafunzi anaweza kubuni jibu* japo, alitoa hoja isiyo sahihi upande wa mapungufu ya maswali hayo kuwa *yanapima sehemu ndogo sana ya maarifa.* Majibu hayo ya watahiniwa yanaonesha kuwa watahiniwa katika kundi hili hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya faida na mapungufu ya maswali ya kuchagua jibu sahihi.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 1,563 (35.9%) waliopata alama 10.5 hadi 15 walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu faida na mapungufu ya maswali ya kuchagua jibu sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alielezea faida za maswali hayo kuwa *ni rahisi kuyasahihisha, maswali haya hayana upendeleo,* na *hupima sehemu kubwa ya maudhui.* Aidha, alieleza mapungufu ya maswali ya kuchagua jibu sahihi kama vile *hayatoi nafasi kwa mwanafunzi kujieleza, maswali haya ni magumu kuyatunga,* na *ni rahisi sana kwa wanafunzi kubashiri jibu*. Mtahiniwa mwingine aliyejibu swali hili kwa usahihi alitoa hoja upande wa faida kama vile *ni rahisi kuyasahihisha, hupima sehemu kubwa ya maudhui,* na *hayatoi nafasi ya upendeleo katika kuyasahihisha*. Pia, alieleza mapungufu ya maswali hayo kuwa *maswali haya ni magumu kuyatunga, maswali haya hayapimi uwezo wa mwanafunzi kujieleza,* na *ni rahisi mwanafunzi kubuni jibu*. Watahiniwa 14 (0.3%) waliopata alama 14.5 na 15 walitumia vyema maarifa na ujuzi walioupata wakati wa mazoezi ya kufundisha hasa katika kutunga na kusimamia mitihani yenye maswali ya kuchagua jibu sahihi. Kielelezo Na. 13.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata ufaulu mzuri katika swali hili.

13


Upimaji ni kitendo cha kutafuta ni kwa namna gani (mtaasisi) Mwanafunzi ameweza kupata maarifa stadi na mielekeo kulingana na malengo talajiwa ya elimu au somo; Upimaji unatumia zana zake katika kumpima mwanafunzi baadhi ya zana hizo ni - Maswali ya kuchagua jibu sahihi, Maswali ya kuchagua jibu sahihi ni aina ya maswali ya jibu fupi ambayo huwa na sehemu kuu mbili sehemu ya swali na vichachawizi jibu huwekwa pamoja na vichachawizi, maswali haya yana zo faida mbali mbali baadhi ya faida hizo ni:-

Hupima sehemu kubwa ya maudhui katika ngazi ya utambuzi, Mwanafunzi ili aweze kuchagua jibu sahihi analazimika kusoma vichachawizi vyote na kuvifanyia kazi ili achague jibu ambalo ni sahihi

Hayatoi nafasi ya upendeleo kwa mwanafunzi msahihishaji, Msahihishaji hawezi kupata nafasi ya kupendelea kwa sababu jibu huwa ni moja ambalo halihitaji kufokasiwa na msahihishaji kwa ni kweli au si jibu sahihi.

Maswali ya kuchagua jibu sahihi, ni rahisi kusahihishwa, Maswali haya hutoa urahisi kwa wasahihishaji kwa kutazama herufi moja tu ambayo inapaswa kusahihishwa.


Tukiacha na na faida za maswali ya kuchagua jibu sahihi maswali haya pia yanazo hasara zake katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, zifuatazo ni baadhi ya hasara hizo ambazo zinaweza kujitokeza kutokana na kutumia maswali haya.


13 Cont.
Ni rahisi kwa wanafunzi kufanya udanganyifu,
wanafunzi wana weza kufanya udanganyifu kwa-
kuangaliziana majibu kwa sababu majibu -
yake ni rahisi mara baada ya kuchaguliwa
na kuwekwa herufi hiyo ni rahisi sana -
mwanafunzi kutazama jibu la mwenzake na-
kupewa jibu na mwenzake.
Maswali ya kuchagua jibu sahihi ni magu-
mu kuyatunga, mwalimu hupitia kazingumu-
kusa anapo weka vitu vya vizi katika swali -
lake hivyo humpotezea muda na asipo kuwa
makini anaweza kushindwa kutunga swali sahihi na
lenye vigezo.
Humchanganya ~~mwanaf~~ Hayampi mwanafunzi
fursa ya kujieleza, Maswali haya hayatoi nafa-
si kwa mwanafunzi ya kujieleza kutokana na kuo-
taka mwanafunzi achague herufi ya jibu sahihi -
tu.
Hivyo basi ni vyema mwalimu anapo amua
kutunga maswali ya kuchagua jibu sahihi ahaki-
kishe kwa anazingatia umakini wa makini
kwa wanafunzi ili kuweza kuepuka udanganyi-
fu.

**Kielelezo Na. 13.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 13.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa ulibaini kuwa watahiniwa 636 (14.6%) waliopata alama 0 hadi 5.5 hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu manufaa na mapungufu ya maswali ya kuchagua jibu sahihi hivyo, walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi. Watahiniwa waliopata alama 0 na 0.5 walitoa hoja dhaifu na zisizo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa utangulizi ambao ni dhaifu na kueleza faida zisizo sahihi za maswali ya kuchagua jibu sahihi kama vile *mwanafunzi kuwa mdadisi, humsaidia mwalimu na mwanafunzi kufikia malengo,* na *huwa na jibu moja kila swali.* Kwa upande wa mapungufu, alieleza hoja mbili badala ya tatu ambazo ni *hupoteza muda* na *jibu huwa sio la moja kwa moja.* Mtahiniwa mwingine alieleza faida zisizo sahihi za maswali ya kuchagua jibu sahihi kama vile *huwa rahisi kueleweka kwa mwanafunzi*, *huokoa muda kwa mwanafunzi wakati wa ujibuji wa maswali haya,* na *humpa mwanafunzi matumaini kwa kujua maswali yanayompa uhakika wa kupata zaidi*. Kwa upande wa mapungufu ya maswali ya kuchagua jibu sahihi, mtahiniwa huyo alitoa hoja zisizo sahihi kama vile *baadhi ya maswali huficha sana maana ya swali, mwanafunzi kuchagua machaguo mawili ya majibu yaliyokaribiana sana au yenye mfanano*

*kujaza kwenye swali moja,* na *baadhi ya maswali hayana herufi ya jibu sahihi katika machaguo*. Majibu ya watahiniwa hao yanaonesha kuwa hawakuwa na maarifa kuhusu faida na mapungufu ya maswali ya kuchagua jibu sahihi. Aidha, watahiniwa wengine hawakuelewa matakwa ya swali kama inavyoonekana katika sampuli ya majibu ya mmoja wa watahiniwa katika Kielelezo Na. 13.2.


13


Upimaji, Ni Kitendo cha Kumwelewasha mwanafunzi.
Kwa njia ya maswali, Zifuatazo Ni hasara Kwamwanafu
nzi. na mwalimu.
Mwalimu na mwanafunzi Kuto kupata Jibu sa
hihi; pio hupelekea mwanafunzi na mwalimu
Kukosa majibu sahihi ya maswali ya kuchagua
na kushindwa kupata Jibu lililo Sahih. kabisa
na kujaza majibu ya uwongo.
Maswali kutoendana na majibu, Pia hupe
lekea maswali kutoendana na majibu sahili na mwali
mu na mwanafunzi kukosa majibu ya kujibia
yale maswali pio ~~mawapa~~ ~~It~~ maswali yasipo endana
na majibu hupelekea lisiendane na majibu na walimu
wakakosa majibu na kushindwa kujibu maswali.
Kufanana kwa majibu, pio hupelekea
Kufanana kwa majibu mfano swali moja kwa
na majibu mawili hupelekea hasara na kushindw
a kujibu Vizuri maswali mbalimbali, Zifuatazo
ni faida za maswali ~~na majibu~~ ya kuch
agua helufi ya jibu sahihi
Kuendana kwa maswali na maji
bu, pio husaidia kuendana kwa maswali
na majibu husaidia mwanafunzi kujibu Vizuri ma
swali na ~~[illegible]~~ anayo pewa na kuweza kukamilisha
Upatikanaji wa majibu kwa uhalaka,
pia inampelekea mwanafunzi au mwalimu
kupata majibu kiuhalaka zaidi na kuweza
kujibu Vizuri maswali na kupata
majibu yaliyo sahihi zaidi.
pio humpelekea mwalimu kutambua swali
na Jibu lake kufasaha Zaidi.

**Kielelezo Na. 13.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 13.

Katika Kielelezo Na.13.2, mtahiniwa alieleza dhana ambazo ni mchanganyiko wa mambo yasiyoleta maana yoyote badala ya kueleza faida na mapungufu ya maswali ya kuchagua jibu sahihi.

### 2.2.4 Swali la 14: Taaluma ya Ualimu

Swali hili lilimtaka mtahiniwa atoe hoja sita zinazoeleza umuhimu wa walimu wa elimu ya msingi kujiendeleza kitaaluma. Jumla ya watahiniwa 4,354 (100%) walijibu swali hili. Takwimu za ufaulu wa watahiniwa katika swali hili zinaonesha kuwa watahiniwa 192 (4.4%) walipata alama 0 hadi 5, watahiniwa 1,898 (43.6%) walipata alama 6 hadi 10, na watahiniwa 2,264 (52%) walipata alama 10.5 hadi 14. Hakuna watahiniwa waliopata alama zote 15. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 14.




**Chati Na. 14:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 14*

Chati Na. 14 inaonesha kuwa asilimia 4.4 ya watahiniwa walipata alama 0 hadi 5, asilimia 43.6 walipata alama 6 hadi 10, na asilimia 52 walipata alama 10.5 hadi 14. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa asilimia 95.6 ya watahiniwa walipata alama 6 hadi 14.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 2,264 (52%) waliopata alama 10.5 hadi 15 walieleza kwa usahihi umuhimu wa walimu wa elimu ya msingi kujiendeleza kitaaluma. Pia, watahiniwa hao walikuwa mahiri katika uandishi wa insha kuanzia utangulizi hadi hitimisho. Kwa mfano, mtahiniwa mmojawapo katika kundi hili alitoa hoja sahihi kama vile *hukuza ubunifu katika kufaragua na kutengeneza zana, hukuza ujuzi na maarifa katika kufundisha, hukuza uelewa na fikra, huwasaidia kujua namna ya kukabiliana na changamoto katika kutekeleza majukumu ya kazi yao, huwasaidia walimu kupanda madaraja na vyeo,* na *huwasaidia walimu kujua mambo mengi na mapya yanayohusu kazi zao.* Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu umuhimu wa walimu wa elimu ya msingi kujiendeleza kitaaluma na hivyo, kupata alama za juu. Kielelezo Na. 14.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.

**14**

Kujiendeleza kielimu ni kitendo cha mtu kuweza kuongeza maarifa, ujuzi, stadi baada ya kuhitimu ngazi fulani ya elimu. Kujiendeleza kielimu kwa walimu wa shule za msingi ni kitendo cha mwalimu aliyehitimu ngazi ya elimu ya msingi kuweza kuendelea au kujiendeleza katika ngazi za juu zaidi ili kukuza ubunifu na ujuzi wa elimu yake. Kujiendeleza kielimu kwa walimu wa elimu ya msingi kuna manufaa yafuatayo;

Hukuza ubunifu katika kufaragua na kutengeneza zana; Kujiendeleza kwa walimu wa elimu ya msingi huweza kuwasaidia kuwa na ujuzi mkubwa katika kubuni kufaragua na kutengeneza zana za ufundishaji na ujifunzaji.

Hukuza ujuzi na maarifa katika kufundisha; Mwalimu aliyehitimu elimu ya msingi anapojiendeleza kielimu huweza kumuongezea maarifa na ujuzi juu ya mbinu, njia na matumizi ya zana katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

Hukuza uelewa juu ya mambo mbalimbali yanayohusu ufundishaji; Kujiendeleza kielimu kwa walimu wa elimu ya msingi huwawezesha walimu kujua na kufahamu mambo mbalimbali yanayohusiana na ufundishaji mfano, namna ya kukabiliana na Changamoto za kufeli kwa wanafunzi n.k.

Huwasaidia kujua namna ya kukabiliana na changamoto katika kutekeleza majukumu ya kazi yao; Hii hutokea sana kwa walimu waliokwisha kuajiliwa wanapojiendeleza kielimu huweza kujua kwa kina zaidi namna ya kukabiliana na changamoto wakati wa kutekeleza majukumu yao.

Huwasaidia walimu kupanda madaraja na vyeo; Mwalimu wa elimu ya msingi anapojiendeleza huweza kumsaidia kupandishwa madaraja ya malipo vile vile kupandishwa vyeo ili kuweza kuendana na elimu yake baada ya kujiendeleza.

**14 Cont.**

Huwasaidia walimu kujua mambo yanayohusu mfumo wa elimu unavyohusiana na mfumo wa siasa ya nchi; Walimu wanapojiendeleza kielimu katika ngazi za juu zaidi huwasaidia kuwa na uelewa mkubwa kuhusiana na mfumo wa elimu pamoja na siasa ndani ya nchi.

Hivyo basi; kwa walimu wa elimu ya msingi wanapojiendeleza kielimu huweza kuleta manufaa nchini kwa kuongeza ubora wa elimu kwa wanafunzi kutokana na kufundishwa na walimu waliojiendeleza ambao huwa na maarifa mengi kuhusiana na ufundishaji wake kwa wanafunzi.

**Kielelezo Na. 14.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 14.


Kwa upande mwingine, watahiniwa 1,898 (43.6%) waliopata alama 6 hadi 10 walitoa hoja pungufu na baadhi ya maelezo hayakuwa na uhusiano na swali. Watahiniwa wengine walitoa hoja zenye kujirudia hivyo, kupata alama za wastani. Kwa mfano, mtahiniwa mmojawapo alifafanua umuhimu wa walimu wa elimu ya msingi kujiendeleza kitaaluma kwa kutoa hoja kama vile *kupanua ufahamu wa kielimu, kupanda ngazi za juu kielimu, kuongezeka kwa mshahara, kuongeza maarifa,* na *kupanua wigo wa kupata ajira*. Katika majibu yake, hoja ya *kupanda ngazi za juu kielimu* alishindwa kuitetea kwa ufasaha na hoja zilizobaki kushindwa kuzitolea maelezo ya kutosheleza. Mtahiniwa mwingine aliyepata alama za wastani katika swali hili alitoa hoja pungufu bila ya kuzitolea maelezo fasaha kama vile *ili kupata stadi mpya, ongezeko la mshahara, kupata wataalamu waliobobea kiufanisi,* na *kupanda daraja*. Katika hoja alizotoa, hoja ya nne ni marudio ya hoja ya pili. Mtahiniwa mwingine alitoa hoja zenye kujirudia kama vile *kukuza taaluma, kupanda daraja, kukuza cheo, kukuza ujuzi na ubunifu, kuongeza maarifa,* na *kuongezeka mshahara.* Katika maelezo yake, hoja ya tatu na ya sita ni marudio ya hoja ya pili. Majibu hayo yanadhihirisha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya umuhimu wa walimu wa elimu ya msingi kujiendeleza kielimu.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 192 (4.4%) waliopata alama 0 hadi 5.5 walikuwa na maarifa kidogo kuhusu umuhimu wa mwalimu wa shule ya msingi kujiendeleza kitaaluma, hivyo, waliandika angalau utangulizi na hoja chache ambazo walishindwa kuzielezea. Watahiniwa 30 (0.7%) waliopata alama sifuri hawakuwa na maarifa kuhusu dhana ya taaluma ya ualimu. Hivyo, waliandika utangulizi usioendana na swali na walitoa hoja zisizo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmojawapo alifafanua hoja kama vile *kuwashauri namna ya kutunza mazingira ili kuweza kupata chakula, hewa safi, kivuli; madawa mbalimbali ya kutibu matumbo kama vile mwarobini; kuwashauri watu kupanda miti ili kuwavutia watalii; kuwashauri namna ya kukabiliana na uchomaji misitu ovyo kwa kuwapa elimu kuhusiana na mabadiliko ya hali ya hewa; kuwashauri wananchi namna ya kutunza rasilimali na mazingira;* na *kuwashauri wanachi kupunguza uchimbaji wa madini kwa kutumia teknolojia duni*. Mtahiniwa mwingine alitoa hoja zisizo sahihi kama vile *nitaanza na utangulizi, nitaeleza maana ya kujiendeleza, nitaeleza aina za kujiendeleza kitaaluma, nitaeleza faida za kujiendeleza, nitatoa shukurani,* na *mwisho nitahitimisha.* Isitoshe, mtahiniwa mwingine alitoa hoja zisizo sahihi kama vile *mwalimu ni kioo cha jamii, mwalimu ni kiongozi, taaluma ya mwalimu, tabia na haiba za walimu, mavazi,* na *kufukuza ujinga*. Mifano yote hii ni ya majibu ya kukosa jambo linaloashiria kuwa

watahiniwa hawakuelewa matakwa ya swali. Kielelezo Na.14.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye hakujibu ipasavyo swali la 14.

14

Hotuba: Ni masimulizi mafupi
yaliyoandaliwa kwa ajili ya kueleza
kitu fulani. Kifuatacho ni hoja kuhusu
mambo nitakayoeleza katika hotuba iliyo-
andaliwa katika kongamano litakalofanyika
katika kijiji cha jirani kama ifuatavyo:-
Dhana ya rasilimali; Hili ni jambo
ambalo nitaweza kuwaeleza walimu wa Elimu
ya msingi kujiendeleza kielimu katika konga-
mano litakalofanyika katika kijiji cha jirani
kwa kuwaeleza dhana ya rasilimali.
Umuhimu wa kutunza rasimali;
Hili ni jambo lingine mojawapo la kuwa-
elezea walimu wa elimu ya msingi kujiend-
eleza kielimu katika kongamano, kwa
kuwaelezea umuhimu au faida zinazo-
tokana na rasilimali.
Hasara zinazotokana na rasilimali
Hili ni jambo mojawapo la kuwaelezea
walimu wa elimu ya msingi katika kuji-
endelezea kielimu kwa kuwaelezea hasa-
ra zinazoweza kutokana na rasilimali
mbalimbali.
Njia za kuanzisha rasilimali;
Hili ni jambo mojawapo la kuwaelezea wa-
limu wa elimu ya msingi katika ku-
anzisha rasilimali kwa kuwaelezea mb-
inu au njia zinazotakiwa kutumika
wakati wa mchakato huo.
Vifaa vitakavyotumika katik-
a kuanzisha rasilimali. Hili ni jambo
mojawapo la kuwaelezea walimu wa


14 Cont. ~~Shule~~ elimu ya msingi kwa kuwaelezea kuwa ni ufaa vipi vitakavyotumika kati-ka kuanzisha rasilimali hizo.
Malengo ya kuanzisha rasilimali; Hili ni jambo mojawapo la kuwaelezea walimu wa elimu ya msingi kuwa wa-kati wa kuandaa na kuanzisha rasilima-li ni lazima uwe na malengo fulani ya kuanzisha rasilimali hizo.
Hivyobasi; Haya ni mambo ambayo nitaweza kuwaelezea walimu wa elimu ya msingi, kujiendeleza kielimu katika konga-mano le litakalofanyika katika kijiji cha jirani kwa kuwaelezea umuhimu au faida zina-tokana na rasilimali hizo husika.

**Kielelezo Na. 14.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 14.

Katika Kielelezo Na. 14.2, mtahiniwa alifafanua dhana ya uwepo wa uanzishwaji wa rasilimali badala ya kufafanua umuhimu wa walimu wa elimu ya msingi kujiendeleza kitaaluma.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA MADA

Kati ya mada tisa (9) zilizotahiniwa katika somo la Ualimu, mada tano (5) zilikuwa na ufaulu mzuri. Mada hizo ni *Uongozi wa Elimu Tanzania (*99.8%), *Ufundishaji* (98.4%), *Taaluma ya Ualimu* (95.6%), *Mtaala* (83.2%), na *Ushauri na Unasihi* (80.9%). Aidha, mada za *Mtaala* na *Uongozi wa Elimu Tanzania* zimekuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo. Kwa upande mwingine, mada mbili (2) za *Upimaji katika Elimu* na *Elimu ya Watu Wazima* zilikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu cha 43.4% na 41.2% mtawalia. Vilevile, mada za *Makuzi na Ukuaji wa Mtoto* (26.3%) na *Nadharia za Kujifunza* (0.4%) zilikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu. Muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa katika mada zilizotahiniwa umewasilishwa katika Kiambatisho cha Pekee.

Ufaulu mzuri kwenye somo hili umetokana na watahiniwa wengi kuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu mada zote zilizotahiniwa katika mtihani wa mwaka 2023, isipokuwa mada za *Nadharia za Kujifunza* na *Makuzi na Ukuaji wa Mtoto.*

## 4.0 HITIMISHO

Kiwango cha ufaulu katika mada zilizotahiniwa mwaka 2023 kilikuwa kizuri kwani asilimia 99.86 ya watahiniwa walipata asilimia 40 hadi 78. Aidha, ufaulu wa mwaka 2023 umepanda kwa asilimia 0.01 ikilinganishwa na ufaulu wa mwaka

2022 ambapo asilimia 99.85 ya watahiniwa walifaulu. Watahiniwa wengi wenye ufaulu mzuri walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha katika dhana mbalimbali zilizoulizwa, uwezo mzuri wa kubaini matakwa ya maswali na ujuzi wa kutosha juu ya uandishi sahihi wa insha. Hata hivyo, watahiniwa walishindwa kupata alama za juu kwa sababu ya kuandika hoja zenye kujirudia, kutoa hoja pungufu na uwezo mdogo wa kufafanua hoja hasa katika maswali ya insha. Sababu nyingine ni kutokuwa na maarifa ya kutosha juu ya dhana mbalimbali zilizoulizwa. Hivyo, watahiniwa walitoa hoja dhaifu.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuendeleza kiwango cha ufaulu katika mada zilizofanya vizuri na kuboresha ufaulu katika mada zenye ufaulu wa wastani na hafifu, mambo yafuatayo yanapendekezwa;

(a) Kutumia mbinu ya majadiliano katika vikundi na mawasilisho kuhusu nadharia za wanafalsafa mbalimbali katika elimu hasa matumizi ya nadharia za ujifunzaji ili kuwajengea wanafunzi uwezo wa kuzitumia katika mazoezi ya ufundishaji. Pia, ni vema wakufunzi wakaandaa igizo dhima ili walimu tarajali wajifunze zaidi kwa vitendo nadharia mbalimbali za ujifunzaji.

(b) Wakufunzi wasisitizwe kutumia makala mbalimbali na utafiti wa maktaba mtandao kuhusu nadharia za kujifunza ili kuboresha ujifunzaji na kuimarisha ufaulu katika mada ya *Nadharia za Ujifunzaji*.

(c) Kutumia mbinu ya mdahalo, mabango yahusuyo ukuaji wa mtoto, chati za hatua za ukuaji wa mtoto na picha zinazoonesha ukuaji wa mtoto zitumike katika kuimarisha ujifunzaji wa athari za mazingira na urithi katika ukuaji wa mtoto ili kuinua kiwango cha ufaulu katika mada ya *Makuzi na Ukuaji wa Mtoto*.

(d) Wakufunzi watoe mazoezi ya kutosha kwa wanachuo wao na kutoa mrejesho wa haraka ili kuwajengea uwezo wa namna bora ya kujibu maswali.

(e) Wakufunzi wapewe mafunzo kazini yanayowajengea uwezo wa kufundisha vizuri mada za *Makuzi na Ukuaji wa Mtoto* na *Nadharia za Kujifunza.*

*Kiambatisho cha pekee*

## UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA ZA SOMO LA UALIMU

| Na. | Mada | Namba ya Swali | Asilimia ya Ufaulu | | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Ufaulu katika kila swali (%) | Wastani wa ufaulu katika kila swali (%) | |
| 1. | Uongozi wa Elimu Tanzania | 10 | 99.8 | 99.8 | Vizuri |
| 2. | Ufundishaji | 5 | 98.4 | 98.4 | Vizuri |
| 3. | Taaluma ya Ualimu | 14 | 95.6 | 95.6 | Vizuri |
| 4. | Mtaala | 9 | 98.9 | 83.2 | Vizuri |
| | | 12 | 67.5 | | |
| 5. | Ushauri na Unasihi | 1 | 89.9 | 80.9 | Vizuri |
| | | 2 | 71.8 | | |
| 6. | Upimaji katika Elimu | 3 | 13.6 | 43.4 | Wastani |
| | | 4 | 20.9 | | |
| | | 8 | 53.5 | | |
| | | 13 | 85.4 | | |
| 7. | Elimu ya Watu Wazima | 6 | 41.2 | 41.2 | Wastani |
| 8. | Makuzi na Ukuaji wa Mtoto | 11 | 26.3 | 26.3 | Hafifu |
| 9. | Nadharia za Kujifunza | 7 | 0.4 | 0.4 | Hafifu |